# *Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu*

(. . .?. . .Nilijaribu kukupigia simu alasiri ya leo, sana nilivyoweza, hukuwa nyumbani nilipojaribu kukupigia. Hei, iwapo una ujumbe endelea nami nitangojea tu. Una hakika, sasa? Huna chochote cha kuhubiri . . .?. . .)

[Ndugu Neville anasema, "Tuna furaha sana usiku wa leo. Ndugu Branham alikuwa tu akiniuliza kama nilikuwa na ujumbe; hakuwa amenipata. Bali haimbidi kunipata. Amina. Nina furaha, usiku wa leo, kwa kuwa nilisema nilichukulia kuwa ni heshima kubwa sana kwamba yeye hata yupo hapa. Na mimi nimesisimkwa, zaidi ya kitu chochote nilichopata kwa ajili ya Krismasi, kujua ya kwamba yeye yupo hapa. Na kwa hiyo Bwana na ambariki anapokuja usiku wa leo. Kama tu alisimama hapa, ingekuwa ni sawa. Bwana asifiwe! Bali nina furaha kwamba yeye yupo hapa, na Bwana ambariki wakati akija."—Mh.]

Asante, Ndugu Neville. Asante.

2 Habari za jioni, marafiki. Nilikuwa nikimwambia Ndugu Neville, ni—nilijaribu kumpigia simu nyumbani mwake alasiri ya leo. Niliwaambia watu kutoka Georgia, na karibu, juma lililopita, ya kwamba sikudhania ningekuwa hapa leo, kwa sababu wengi wa watu huja.

3 Na, hata hivyo, kwenye Krismasi, mwajua, watoto wadogo, huwezi kuwaambia vinginevyo. Wao, ninii tu, ni wakati wa Krismasi kwao. Nao wasingetaka maskini soksi zao zitundikwe, kungekuwa na kitu fulani. Ni desturi, hata katika taifa letu, kwamba wanatundika soksi, na kitu kingine. Mbona, nilifanya hivyo, nilipokuwa mtoto, na—na ingawa liko mba—mbali sana na Maandiko, njia iliyowekwa kama lilivyo. Hata hivyo, watoto ni ninii, wanasikia watoto wengine wakisema, "Vema, nilipata *hiki* kwa ajili ya Krismasi. Nilipata *hiki*." Jamaa hao wadogo wanasimama huku, wanaangalia, mwajua. Huwezi, huwezi kuwafanya waelewe. Unaona? Kwa hiyo, kwamba tu, Krismasi itadumu. Naam.

4 Wala siyo siku ya kuzaliwa kwa Bwana wetu, wakati Yeye alipozaliwa. Sasa, kama utaenda kwenye ninii yako. . .duniani, na kuangalia, Yuda iko mbali chini ya ikweta kadiri tu hii ilivyo juu yake. Kwa hiyo tunaona, huko Yuda, kwenye hiyo milima huko juu, kwamba kuna theluji. Jamani! Kunayo theluji nyingi kuliko kulivyo huku. Kwa hiyo wale wachungaji wasingeweza kuwa kwenye. . .juu ya mlima wakati huo, wakichunga kondoo wao.

5 Na jambo lingine, Yeye, ingekuwa ni kinyume na maumbile yote. Mnaona? Wana-kondoo na kadhalika huzaliwa kwenye msimu wa kuchipusha majani, si wakati huu wa mwaka. Wana-kondoo hawazaliwi sasa. Ko—kondoo jike hawazai sasa. Naye alikuwa ni Mwana-kondoo wa Mungu, mnaona. Kwa hiyo pale, Yeye alizaliwa kwenye, wanadai, wakati fulani Aprili, katikati ya Aprili, kitu kama hicho.

6 Lakini, hii ikiwa ni tarehe 25 Desemba, mbona, wakiifanya siku ya kuzaliwa. Hii ni siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua. Mnaona? Baalimu wa Kirumi, mungu-jua. Mnaona? Nalo jua liko katikati ya mzunguko sasa. Na kuanzia tarehe 20 hadi tarehe 25 ilikuwa ndiyo wakati sarakasi za Kirumi zilikuwa zikiendelea, katika kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua. Na kwa hiyo wakasema, "Vema, sasa, kuwafurahisha Wakristo na wapagani pia, tutafanya, badala ya mungu-jua, Mwana wa Mungu na mungu-jua, pamoja. Kwa hiyo tutazichanganya zote pamoja na kufanya siku ile ile ya kuzaliwa, na tuifanye iwe tarehe 25." Kwa hiyo ilionekana kuwafurahisha makafiri na kanisa la kawaida wakati huo, kwenye kanisa la kwanza la Kirumi. Ilikuwa ni ninii tu. . . Ilikuwa tu ni sawa kwao, kwa hiyo hawakujali. Kwa hiyo wakaifanya siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua na ya Mwana wa Mungu.

7 Sasa, siku ndefu kuliko zote katika mwaka ni kwenye tarehe 21 ama tarehe 22, usiku ulio mrefu kuliko wote, namaanisha, katika mwaka, ni kwenye tarehe 21 ama tarehe 22, wakati, katika mfumo wa jua, jua ndio kwanza lirudi, likirudi. Sasa zitaanza kupata sekunde chache tu ama dakika zaidi. Halafu basi wakati fulani Juni ama Julai, tunao mchana ulio mrefu kuliko wote katika mwaka.

Kwa hiyo, lakini, Krismasi itadumu, kwa hiyo ha—hatuwezi kuiepuka.

8 Tairi zisizo na tyubu zitaendelea kuwepo. Ninazichukia, bali zita—zitaendelea kuwepo. Uh-huh. Hiyo ni kweli.

9 Wanawake walio uchi, wataendelea kuwepo. Kaptura, zitaendelea kuwepo. Hivyo tu. Zitaendelea kuwa fupi wakati wote, kwa hiyo hakuna kitu ninachoweza kufanya juu yake.

Ninasema tu ni kosa. Kaa na Hilo, na hiyo ni sawa.

10 Dhambi, itaendelea kuwepo. Itaendelea kuwepo. Tutakuwa nayo, kuendelea na kuendelea. Kwa hiyo, ninii tu, itaendelea kuwepo hata Yesu atakapokuja. Na mambo haya yote yataendelea kuwepo. Sasa, siamini. . .

11 Hebu nilifanye hili dhahiri. Siamini ya kwamba Yesu angejali ni siku gani uliiabudia siku ya kuzaliwa Kwake, kama ni tarehe 25, 26, ama kama ni Aprili, Mei, Juni, Julai, ama wakati wowote iwezao kuwa, mradi tu unaabudu, wewe mwabudu siku yoyote.

12 Lakini jambo ndilo hili. Wameuondoa utakatifu kutoka kwenye Krismasi, kuifanya siyo Krismasi bali, siku ya kuabudia, bali sherehe. Mnaona? Hatuninii . . . Mnawasikia watu wakisema, "Tutasherehekea Krismasi." Hilo ni kosa. Kamwe hatupaswi kuisherehekea Krismasi. Krismasi ni siku ya kuabudia, sio sherehe.

13 Tunaisherehekea siku ya kuzaliwa kwa Lincoln. Tunaisherehekea siku ya kuzaliwa kwa Washington. Kama ulikuwa huko chini kabisa Kusini, tungeisherehekea siku ya kuzaliwa kwa Lee, ama—ama Jackson. Siku yao ya kuzaliwa ni sherehe.

14 Bali siku ya kuzaliwa kwa Kristo, ninaamini, inapaswa kuwa ni siku ya kujiweka wakfu, kuabudu, badala ya usiku wa leo. Watu kanisani, magotini mwao, wakiomba, wakimshukuru Mungu kwa ajili ya Zawadi halisi ya Krismasi.

15 Viatu vyenye visigino virefu, na nyuso zilizopakwa rangi, na makoti marefu, na bilauri za wiski zitainamishwa, moja kwa nyingine. Na wiski yenye thamani ya maelfu mara maelfu ya dola, na biri, na sigara zitasambazwa usiku wa leo. Wakati, maelfu ya watoto wadogo, maskini, wenye njaa wanalala bila ya kitu cha kula wala mahali pa kulaza kichwa chao.

16 Kuabudu, ndiko tunakohitaji. Sherehe ndiyo tuliyo nayo. Loo, hiyo ni sawa. Hiyo, siyo . . . si sawa, bali hatuwezi kuikomesha. Itaendelea kuwepo. Sisi, tutaendelea kuwa na Krismasi moja kwa moja vivyo hivyo.

17 Nalo neno *Krismasi*, Krismasi linatoka kwenye neno "misa ya Kristo," misa ya Kristo, K-r-i-s-m-a-s-i. Mnaona? Misa ya Kristo, ni desturi ya Kikatoliki.

18 Naye nanii wangu mdogo, mmoja wa binti zangu, siwezi kumwita mdogo tena, Becky, alipaswa kuandika hadithi hivi majuzi, juu ya kisasili, juu ya hadithi za kubuniwa. Nami nikasema, "Andika tu juu ya Baba Krismasi." Ndiyo—ndiyo hiyo. Baba Krismasi amepachukua mahali pa Kristo. Naye Baba Krismasi, kamwe hapakuwapo na mtu kama huyo. Mnaona? Kabisa ni desturi ya Kikatoliki, haina uhusiano wowote na Waprotestanti wala chochote kuihusu, mnaona, ama Krismasi, ama kuzaliwa kwa Kristo, hata kidogo. Lakini huyo Baba ataendelea kuwepo.

19 Bali siku moja Yesu atakuja kudumu. Huyo Ndiye tunayemtazamia.

20 Sasa, hakika ningependa Ndugu Neville aichukue mimbara hii, usiku wa leo. Kwa sababu, ni, niliwaambia watu ya kwamba singekuwako leo. Na endapo ningeshuka na kusema lolote, ningenasa kanda. Nami ninatumaini ya kwamba wao . . . Hivi mna kinasasauti kinachoendelea, mnacho? [Mtu fulani anasema, "Naam."—Mh.] Kufanya kanda. Kama Roho Mtakatifu kwenye

wakati wa mkutano alinena lolote, huenda ikawa wangeninii, wangeweza kulisikia. Mnaona?

21 Ninayo Maandiko fulani, na kadhalika, yaliyoandikwa hapa, somo dogo. Wala sijui; ninatumaini kwamba Bwana atalibariki. Lakini jambo ni kwamba, kwa kawaida, kwenye Jumapili hizi usiku, hao jamaa hutoka hapa kufikia yapata saa tatu, ama dakika kumi baadaye, na itakuwa vema kuondoka kabla ya saa saba.

22 Kwa hiyo, bali nadhani kunayo saa. Uh-huh. [Ndugu Neville anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Kitu gani? Kitu fulani, ibada ya usiku wa manane? ["La, sio usiku wa leo, hapa."] Ninamaanisha . . . La, sio usiku wa leo, la. Hilo, a—aliwazia labda nilikuwa nayo, nilichanganyikiwa, huu ni usiku wa Mwaka Mpya.

23 Vema, tunatarajia wakati mkuu, usiku wa Mwaka Mpya. Huo ndio wakati ambapo sisi, kila, ndugu wote huja humu, nasi tunakuwa na ushirika mkuu, sisi kwa sisi, kwenye usiku wa Mwaka Mpya.

24 Sasa, lakini nilikuwa tu nikiwatania kuhusu hilo. Nami natumaini hilo halikuingia kwenye kanda.

25 Aisee, hivi majuzi, nikinasa kanda, nilikigonga kitu *hiki* mara kadhaa, na—na nikaiharibu tu kanda hiyo, juu ya *Ukristo Dhidi Ya Upagani*. Hizo kanda ziliharibika. Kwa hiyo kama kanda zina—zinacheza ama zinaingia, laiti yeyote anayezinasa angekuja mlangoni. Afungue tu mlango ama kitu fulani, nipate kujua ya kwamba sasa inaendelea. Nitaona jinsi kitu *hiki* kitakavyotokea, kama kinaendelea. Sawa. Vema. Hilo ni sawa. Nitakifunika, niende upande huu mwingine. Sikukizoea.

26 Vema, ninataka kuchukua fursa hii kulishukuru kanisa hili na washiriki wake, kwa ajili ya vitu vizuri mlivyonipa kwa ajili ya Krismasi. Muda mfupi uliopita, mwanangu aliingia na kunipa kifurushi kikubwa. Nami nilikuwa katika . . . chumba changu cha kusomea, nikisoma. Nikakifungua, na nikaona suti mpya kutoka kwa maskani hii. Na vitu vidogo vya kibinafsi ambavyo watu wamenitumia, huko juu tu, ambavyo sijafungua mpaka Joe atakapokuja usiku wa leo na kukifungua chake. Halafu basi, bi—bila shaka ninathamini hilo. Bwana awabariki. Laiti ningaliweza kumpa kila mtu zawadi za Krismasi. Siwezi kufanya hivyo. Mnajua jinsi ilivyo. Huwezi tu kufanya jambo hilo. Hivyo tu. Kama wewe—kama ukimpa mmoja, inaonyesha heshima namna hiyo. Kamwe huwezi kulifanya. Mhudumu hawezi kufanya hivyo.

27 Nami nasikia ya kwamba Ndugu Neville, asubuhi ya leo, alipewa koti jipya. Ninawashukuru sana ninyi nyote, kwa ajili ya ndugu yangu.

28 Kunayo siri ndogo kwenye hilo, ambayo mimi na Billy Paul tunaijua. Mwajua, mimi ni mwenda pole sana kuhusu

chochote, mimi . . . kushika, kwa vyovyote, juu ya chochote. Billy aliniambia, hivi majuzi. Akasema, "Unajua, baba, nilikuwa huko kwenye supamaketi. Na," kasema, "ni nani nilikutana naye huko?" Alikuwa na mtetemo mdogo katika sauti yake. "Ndugu Neville, na," akasema, "alikuwa na koti, lilionekana baya sana."

Na mimi nikasema, "Yangu inaweza kumwenea?" Uh-huh.

29 Na kwa hiyo, naye akasema, "La. Yeye ni mtu mkubwa zaidi kuliko ulivyo wewe."

Kwa hiyo nikasema, "Loo, nitashuka niende nikamnunulie moja."

30 Kwa hiyo, ndipo napata hundi yangu kutoka kanisani hapa, kama yeye afanyavyo. Kwa hiyo kwenye wakati huo, Billy akaja mbio na neno kubwa lenye ushawishi, na tabasamu usoni mwake, "Baba, kanisa litamnunulia moja." Vema, ninajua kanisa hakika lingeweza kumnunulia moja zuri kidogo kuliko mimi, kwa hiyo nikawaza, "Hilo ni zuri tu sana, kwa hiyo sote tungepata." Lakini tunajua ya kwamba imekuja katika mahali pazuri sana, ambapo Ndugu Neville anahitaji koti hilo.

31 Mwajua, ninataka kuwaambieni jambo fulani dogo juu ya hilo. Nilikuwa nikisoma kwenye historia. Hivyo ndivyo tu nimefanya majuma machache yaliyopita, miezi ama miwili, imekuwa ni kusoma historia ya Biblia. Wakati mmoja nilisoma ninii . . .

32 Kitabu changu cha kwanza kilikuwa ni Agano la Kale, kile Mungu alichokuwa katika Agano la Kale. Kisha nikachukua Agano Jipya, nami nikaona kile Mungu alichokuwa, kukilinganisha siku hizi, kwa sababu ninajua Yeye hana budi kubaki yule yule. Mnaona?

33 Basi kuna sehemu moja ya kanisa niliyokosa kabisa, hiyo ilikuwa ni ule muda kati ya kuondoka kwa mtume wa mwisho hadi kule kuja kwa wakati wa giza, wakati kanisa Katoliki lilichukua mamlaka. Walipoteza miujiza yote, na Uungu wote, kutoka kanisani, kila kitu. Na mimi—mimi nataka kujua ni kitu gani kilichotukia kwenye wakati huo, kwa hiyo nikachukua tu baadhi ya historia za kale sana zilizopo, kama vile *Babeli Mbili* cha Hislop na *Kanisa Linalosafiri* cha Broadbent, *Kitabu cha Wafia Imani Cha Foxe*, *Wazee Wa Baada ya Nikea*, *Baraza La Nikea*, *Kabla Ya Baraza La Nikea*, na hao wanahistoria wote mashuhuri ambao wameandika kwenye nyakati hizo, maisha ya watu hao wote wa thamani. Nilipovisoma, inaonekana kama ningeweza kusikia *Zaburi Ya Maisha* ya Longfellow:

> Maisha ya watu mashuhuri yote yanatukumbusha
> Tunaweza kufanya maisha yetu adhimu,
> Kwa maagano huacha nyuma yetu
> Kumbukumbu za kudumu.

34 Ninapoona yale hao wanaume na wanawake waliyopitia, huko nyuma, na kuona, kuidumisha Injili ii hii! Na wakati walipoihubiri Injili ii hii, jambo lile lile lililotukia katika Agano la Kale, Agano Jipya, na halafu ni vile vile tu hasa. Kwa hiyo hilo hulipa shahidi mmoja, wawili, watatu. Kila neno linaimarishwa. Mungu yeye yule aliyeshughulika na manabii wa kale, alishughulika na mitume, na akashughulika na wale ndugu wa kabla ya Nikea.

35 Naye huyu hapa leo hii, akishughulika kwa njia ile ile na watu Wake, kwa ishara zile zile, maajabu yale yale, Injili ile ile, nguvu zile zile, Mungu yule yule, kila kitu. Pamoja na watatu kama mashahidi, kwetu sisi, kwamba *Hii* ni Kweli. *Hii* ni Kweli. Mungu aliitoa katika maagano matatu. Mnaona? Historia hiyo ni . . .

36 Biblia ndiyo historia ya yale Mungu aliyokuwa, vivyo hivyo na historia ya Agano la Kale.

37 Agano Jipya ni historia ya—ya Agano Jipya.

38 Na *Baraza la Nikea Na Wazee Wake*, na *Baada Ya Baraza La Nikea,* ni historia ya kanisa basi.

39 Na sasa historia inajiandika tu kama vile ilivyofanya. Ambapo, historia hii haitaandikwa kamwe. La. Kule Kuja kumekaribia sana sasa.

40 Na Mungu na amsaidie mtu katika siku hizi, watu wanaojaribu kutafuta heshima ya wanadamu, wanaume wanaojaribu ku—kujifanya maarufu, ama miongoni mwa wanadamu. Hivi hamjui, kwamba binadamu, inapoangamia, hayo yote huangamia pamoja nayo? "Lakini tafuteni kupata hazina za Mbinguni. Hazitapita kamwe."

41 Baraka za Mungu za thamani sana ziwe juu yenu nyote. Niliwaambia, usiku wa leo, kwa kawaida ni desturi yangu kwenda kanisani mahali fulani Jumapili, kama nikiweza.

42 Mimi, leo hii, asubuhi ya leo, nilitaka kushuka huku sana, na kuusikia ujumbe wa Ndugu Neville. Lakini baada ya kutoa ahadi hiyo, basi sikutaka kuivunja.

43 Kwa hiyo basi nikajaribu kusikiliza redio, na—na kadhalika, na yote niliyoweza kusikia ilikuwa, "Mara baada ya ibada hii, sote tutakutana huko nje kwenye chumba cha chakula cha mchana tunywe kahawa pamoja. Na tutaninii . . ." Kwani kanisa limekuwa nini? Ni chama. Kwa nini msiseme tu "chama" badala ya kanisa. Kanisa halipaswi kufanya hivyo. Kanisa si mkutano wa kunywa kahawa, ama mlo mkubwa wa kutwa, au milo ya jioni, na vitu vya namna hiyo.

44 Tunao ushirika pamoja na Bwana. Kanisa, hapo ndipo tunaposhiriki pamoja na Yeye.

45 Nilimwambia mke, "Mpenzi, ni—ninakuwa mkosoaji sana, ninachukia kuenda huko chini maskanini, ama hata kuingia

mimbarani.” Loo, kadiri ninavyozidi kuzeeka, inaonekana, ndivyo ninavyozidi kuwa mbaya zaidi. Nami si—si—sitaki—sitaki kuwa hivyo, namna hiyo. Bali kuna kitu Fulani ndani yangu kinachonisukuma, kuwa namna hiyo.

46 Kisha nikasema, “Kwani ninaingia wazimu? Kwa nini siwezi kuambatana na umati huo mwingine? Kwa nini siwezi kwenda kama ndugu hao wengine? Kwa nini siwezi kujipatia dhehebu, nilitegemee kama wao wafanyavyo? Ama, kwa nini siwezi kutoka nje na kuacha kuwashambulia watu na vitu kama hivyo? Kwa nini siwezi kufanya hivyo?” Nikasema basi, nafikiri, “Hivi nimeingia wazimu?”

47 Ndipo nikarudi kwenye Neno, na hilo hapo. Sina budi kudumu na hilo Neno.

48 Nikasema, “Mimi, kama isingalikuwa ni kwa ajili ya Neno la Mungu, nami nilijua Mungu yupo, ningalijijengea kibanda kidogo mahali fulani, huko mbali sana katika British Columbia, huko mbali sana Canada, huko milimani ambako nisingemwona mwanadamu, mara moja kwa mwaka. Na huko ningeisikia Sauti ya Mungu katika vijito vyenye mawimbi, na kumsikia wakati Yeye alipopaza sauti, katika mbwa mwitu juu ya mlima. Ningemsikia Yeye wakati akinong’onezea kupitia misonobari mikubwa, na kuuangalia uso Wake wa kupendeza kwenye kioo cha ziwa, hapo kinapoakisi ile milima mikubwa iliyofunikwa na theluji. Mbona, ningemwabudu Mungu kila siku ya maisha yangu, huko nyuma. Ninajua ningekuwa halisi sana kumhusu Mungu, huko nyuma, kuliko niwezavyo nikizisikiliza karamu za kahawa na za chai, na upuuzi wote wa namna hii tulio nao siku hizi, unaojiita kanisa; kanuni za imani, na hadithi za uongo, na hekaya, na kila kitu kingine, kupachukua mahali pa Injili.”

49 Afadhali niyasome Maandiko, sivyo, ndipo tuanze. Sasa, kabla hatujasoma, hebu tuzungumze na Yeye Ambaye aliyaandika, tunapoviinamisha vichwa vyetu.

50 Wote walio na haja usiku wa leo, huu ukiwa ni usiku wa mkesha wa Krismasi, huenda ukawa na kitu kama hiki, “Ee Bwana, ninashukuru moyoni mwangu kwa ajili ya Kristo, nami ninataka kusongea karibu zaidi tu kidogo kuliko hapo awali. Sitaki kurudi horini katika banda, bali ninataka kuufanya moyo wangu hori, sio kwa Kristo aliye mtoto mchanga, bali Kristo aliye Mungu, Imanueli.” Waweza tu kulifanya lijulikane kwa kuinua mkono wako kwa Kristo? Bwana aijalie haja yako.

51 Baba wa Mbinguni, sasa tumekusanyika katika nyumba inayoitwa nyumba ya maombi, mahali ambapo tunakutanika kumwabudu Bwana Yesu katika kazi Zake zote kuu, na kulifundisha Neno Lake, na kuamini kwamba Yeye ni Neno. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya usiku huu, na fursa zake zilizowekwa mbele zetu, kulileta Neno la Mungu aliye hai kwa watu walio hai, na hasa sana kwa wale wanaoishi katika Kristo

Yesu, ambao wamefanywa upya, wamezaliwa upya, wakawa viumbe vipya. Na nafasi tuliyo nayo ya kuwasilisha u—ukweli kwa wale wasio viumbe vipya katika Kristo, ili, usiku wa leo, waweze kuwa viumbe vipya katika Kristo. Mpe kila mmoja wa watu hawa shauku ya moyo wao.

52 Pia wajalie, usiku wa leo, iwapo hawajafanya hivyo hapo kabla, waingie katika Kanisa hili kuu la ulimwengu mzima, katoliki; hili, *katoliki,* kwa kuwa liko "kote ulimwenguni," la kimitume, watakatifu waliozaliwa mara ya pili wa Mungu aliye hai. Tujalie, Bwana. Jalia kila mtu awe ni mshirika Wake. Kwa sababu, ni Mwili, si jengo, bali ni Mwili, Mwili wa Kristo, nasi ni washiriki wa Mwili huu. Tujalie, Bwana.

53 Jalia karama kuu kutoka kwa Kristo zimwagwe juu ya watu, usiku wa leo, walio washiriki wa huu Mwili. Sio kifurushi kilichotiwa muhuri, si kikiwa na zawadi za Krismasi ndani yake, kama vile sisi watu wa duniani tunavyoweza kupeana, kwa kuuthamini upendo wetu mmoja kwa mwenzake. Lakini hebu iwe ni ule muhuri wa Roho Mtakatifu ukishuka chini kwenye nafsi ya mwanadamu, ukiwapa Uzima usiopatikana na mauti. Wabariki wote, pamoja, Baba.

54 Wakati, usiku wa leo, tujuavyo sisi, tukiwa wenye afya na wenye furaha, tukiwa na moto mzuri wenye joto karibu nasi, paa juu ya kichwa chetu, na tukiwazia juu ya maelfu kote ulimwenguni, wasio na mahali pa kwenda. Baba wa Mbinguni, uturehemu sisi, na ulijalie ombi hili.

55 Tunaomba usiku wa leo ya kwamba Wewe utalibariki Neno linapotolewa sasa.

56 Mbariki mchungaji wetu. Wabariki wadhamini na mashemasi wa kanisa, na kila mmoja aliyeshirikishwa nalo, katika uanachama wa huo Mwili, wakiwa wamezaliwa mara ya pili. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

57 Kama nilivyoanza, dakika chache zilizopita, kusema, katika kusoma juu ya wale watakatifu. Mtakatifu Martin alikuja usiku mmoja baridi, akamwona maskini mzee amelala, akiganda, langoni. Naye akawaona watu wakipita hapo karibu, ambao waliweza kumpa huyo mzee jo—joho la namna fulani, bali hawakufanya hivyo. Naye akijua basi kwamba lilikuwa ni jukumu lake kufanya hivyo, japo baba na mama yake ni makafiri. Bali yeye alikuwa askari, kwa hiyo akavua joho lake, akachukua upanga wake na kulikata, nusu, vipande viwili, akamfunga huyo jamaa mzee kwalo, kisha akaenda zake. Ndipo watu wakamcheka, wakamdharau. Kasema, "Askari wa kuchekesha! Ni mlokole wa jinsi gani!"

58 Lakini kesho yake usiku, aliamshwa, huko kambini alikokuwa akikaa, naye alikuwa katika ono. Ndipo akaangalia, naye alikuwa chumbani, na hapo akasimama Yesu pamoja na kundi la Malaika waliomzunguka. Naye Yesu alikuwa

amejifunika kipande hiki cha joho, lile vazi. Ndipo Yeye akawaambia hao Malaika, “Mnajua nilipolipata hili?”

Nao wakasema, “La, Bwana wangu.”

Akasema, “Martin alinifunika na hili.”

59 Kwa hiyo Ndugu Martin akajua, basi, huo ulikuwa ni wito wake kwenye huduma. Kwa sababu, hapo alipomfunika maskini mzee huyo na hilo joho, Yesu alikuwa ndani ya mzee huyo. Kwa hiyo ikiwa Yeye alikuwa ndani ya mzee mmoja, kama vile tungemwita mwombaji ama ombaomba, amelala mtaani, Yesu atamjia yeyote wetu. Ndipo akajua, “Kadiri ulivyomtendea mmojawapo wa walio wadogo wa hawa, watoto Wangu, umenitendea Mimi.” Mungu na atusaidie kukumbuka hilo.

60 Sasa, ninyi mlio na Biblia zenu na mnataka kuandika fungu la maneno, ninataka kusoma mahali pawili kutoka kwenye Maandiko Matakatifu usiku wa leo, moja kutoka katika Isaya, na moja kutoka katika Yohana Mtakatifu. Ninataka kusoma kutoka Isaya, mlango wa 42; na kutoka Yohana Mtakatifu mlango wa 12. Ninataka kuyasoma hayo Maandiko. Isaya 42 inaanza na 1, kifungu cha kwanza, na inateremka hadi kifungu cha 7 vyote pamoja.

> *Tazama mtumishi wangu, nimtegemezaye; mteule wangu, ambaye nafsi yangu imependezwa naye; nimetia roho yangu juu yake: naye atawatolea Mataifa hukumu.*
>
> *Hatalia, wala hatapaza sauti yake, wala kufanya isikiwe katika* njia kuu.
>
> *Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima: atatokeza hukumu kwa kweli.*
>
> *Hatazimia wala hatakata tamaa, hata atakapoweka hukumu duniani: na visiwa vitaingojea sheria yake.*
>
> *Hivi asema . . . BWANA, yeye aliyeziumba mbingu, na kuzitanda; yeye aliyeitandaza nchi na . . . mazao yake; yeye awapaye pumzi watu walio juu yake, yeye awapaye roho wao waendao ndani yake:*
>
> *Mimi, BWANA, nimekuita katika haki, nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya Mataifa;*
>
> *Kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa* kwenye gereza, *kuwatoa* magerezani *waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani . . . nyumba ya kufungwa.*

61 Sasa katika mlango wa 12 wa Yohana Mtakatifu, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 17 na kusoma . . . kufikia yapata kifungu cha 28.

> *Basi wakamshuhudia wale . . . waliokuwapo pamoja naye, alipomwita Lazaro kutoka kaburini, akamfufua.*

*Na kwa sababu hiyo mkutano walikwenda kumlaki, kwa kuwa wamesikia ya kwamba amefanya ishara hiyo.*

*Basi Mafarisayo wakasemezana wao kwa wao, Mwaona kwamba* sisi *hatufai neno lolote? tazameni, ulimwengu* umekwenda *nyuma yake.*

*Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:*

*Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*

*Filipo akaenda, akamwambia Andrea: kisha Andrea na Filipo* wamwambia *Yesu.*

*Naye Yesu akawajibu, akasema, Saa imefika atukuzwe Mwana wa Adamu.*

*Amin, amin, nawaambia, Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake: bali ikifa, hutoa mazao mengi.*

*Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele.*

*Mtu akinitumikia, na anifuate;* (sikilizeni sasa) *nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo: mtu akinitumikia, Baba atamheshimu.*

*Sasa roho yangu imefadhaika;. . .nisemeje? Baba, niokoe katika saa hii: lakini ni kwa* (sababu) *ajili ya hayo nilivyoifikia saa hii.*

*Baba, ulitukuze jina lako. Basi ikaja sauti kutoka mbinguni, ikisema, Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena.*

62 Sasa, ninatoa kutoka kwenye hili, somo ambalo nimelitumia katika njia nyingine: *Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.*

63 Mara nyingi hapo awali, nimeliendea somo hili, na, ila tofauti kidogo na vile ninavyotarajia kufanya, usiku wa leo. Sasa, huu ni mkao usio wa kawaida wa mandhari ya ujumbe wa Krismasi. Lakini nadhani, leo hii, ninyi, kwenye redio, mmesikia *Watu Watatu Walio Wa Mashariki* na *Mji Mdogo wa Bethlehemu,* na *Usiku Mtulivu*, na kuwasikia wahudumu wakinena juu ya kuzaliwa Kwake, na kadhalika. Nami, huku nikiuweka Ujumbe wangu wa Krismasi usiku wa leo, mkiisha kuwa na mengi sana yake alasiri ya leo, na siku mbili ama tatu zilizopita, niliwazia ningechukua mwelekeo tofauti wake, sio kutoka kuzaliwa Kwake, nami ningelizungumzia kwa njia nyingine. Na mkao huu usio wa kawaida kabisa, bali ni katika

mambo yasiyo ya kawaida ambako tunaona Ukweli wa Neno la Mungu. Ni katika jambo lisilo la kawaida.

64 Ilikuwa ni katika mkao usio wa kawaida wa Neno la Mungu, ambapo watu walimtambua Yeye kwamba ni Masihi, sio mkao wa kawaida ambapo Mafarisayo na Masudukayo walikuja, wakiwaambia. Lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida, kumwona Masihi akizaliwa katika banda, badala ya kushuka kutoka ushoroba wa Mbinguni, kama walivyodhania Yeye angekuja, ama kama wao—wao walisema Yeye angekuja.

65 Lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida, wakati, kwenye mto Yordani, wakati "milima ilirukaruka kama wanakondoo," na mjumbe kutumwa mbele Zake. Badala ya yeye kuwa kuhani aliyestaarabika vizuri ambaye angekuja kukutangaza kuja Kwake, wangemwona mtu mwenye masharubu kote usoni mwake, na nywele za matimutimu, huku amezungushiwa kipande cha ngozi ya mnyama, kama kabuti. Kisha anatembea matopeni, yaliyomfikia juu ya tindi za miguu yake, labda, na kuhubiri ujumbe wa kuchangamsha sana. Kisha kuwaambia Mafarisayo na Masadukayo, na kuwaita hao wanachuoni, "Enyi kizazi cha nyoka." Hilo lilikuwa lisilo la kawaida kwa mtu kufanya hivyo, bali ilikuwa pia ndiyo njia ya kuupata Ukweli, Uzima, njia isiyo ya kawaida. Sio njia ya kawaida, iliyoandaliwa, bali njia isiyo ya kawaida.

66 Na ni shauku ya moyo wangu usiku wa leo, ya kwamba, katika Andiko hili lisilo la kawaida, kwamba tutapata maana ya kweli ya Krismasi, kile Krismasi inachomaanisha kwetu, jinsi tunavyopaswa kuifanya sasa, ama yale, jinsi inavyotupasa kuiendea Krismasi.

67 Sasa tunaona hapa ndani, kama vile tumesoma, Wayunani hawa walitaka kumwona Yeye. Walikuja kumtafuta Yesu. Hapana shaka kwamba wao, kama vile mimi na wewe, walikuwa wamesikia juu Yake, yale matendo makuu ambayo alikuwa amefanya, na yale mahubiri makuu aliyokuwa amehubiri, na mambo yasiyo ya kawaida ya maisha Yake, kwa hiyo akawa ni Mtu asiye wa kawaida.

68 Nami napenda kusimama hapa muda mrefu tu wa kutosha kusema hili, kwamba, karibu sikuzote, unapompata Mungu ndani ya mtu, unamwona mtu asiye wa kawaida kabisa akitumiwa katika njia isiyo ya kawaida kabisa.

69 Kwa hiyo, Yesu alikuwa ni Mtu wa aina hii, na Yeye aliwavutia watu, wapate kujua Yeye alikuwa nini na alikuwa ni Nani.

70 Na, bila shaka, Wayunani hawa walikuwa ni wapagani, makafiri, kwa sababu Wayunani waliabudu sanamu. Nao walikuwa ni wakuu, vema, ningesema, wachonga sanamu na wanariadha. Nao walikuwa na sanaa nyingi, Wayunani walikuwa nazo, sanaa kuu za Kiyunani, ambazo hazijapata

kushindwa hata wa leo, sanaa zao. Nao walikuwa ni watu wakuu, wanariadha.

71 Basi wakiwa, wakijua kwamba kulikuwako na Mungu mahali fulani. Nao walikuwa na maelfu yao waliyoabudu. Nao walikuwa wamesikia juu ya Mungu wa kihistoria ambaye alifanya miujiza mikubwa miongoni mwa Waebrania. Halafu walikuwa pia wamesikia ya kwamba Mungu huyu, aliyekuwa ni Mungu mfanya miujiza wa Kiebrania, alikuwa huko kwenye nchi yao, pamoja nao tena. Kwa hiyo ikauvutia usikivu wao, basi wakaja kumwona Yesu.

72 Basi angalieni, kwa kawaida jinsi watu wanavyotaka kumwona Yesu, ni kumpata mtu fulani ambaye anajua jinsi ya kuwapeleka Kwake. Kiongozi, ama mmoja wa watumishi Wake, ndivyo wanavyompata Yeye. Kwa hiyo Yesu, kama akiwahi kumchagua mtumishi, Yeye sikuzote humchagua mtu atakayewaleta watu Kwake, kwa sababu ni kusudi Lake kuwatumikia watu.

73 Sasa tunaona ya kwamba waliletwa Mbele Zake. Sasa, Wayunani hawa. Filipo, walikuwa wameshauriana na Filipo, naye Filipo akasema, "Sasa, huyu hapa mtu fulani anayetaka kumwona Bwana wetu. Kwa hiyo isingekuwa ni sawa tu kwangu kupata heshima ya kuwatambulisha Wayunani hawa kwa Bwana wangu, kwa hiyo nitaenda nimchukue Andrea aende pamoja nami." Kwa hiyo wakaenda wakamchukua Andrea. Naye Andrea na Filipo, wote wawili, wakaja na—na kuwakabidhi Wayunani hawa kwa Yesu.

74 Sasa, hili hapa jambo kuu, na ni somo lisilo la kawaida. Mara Wayunani hawa walipoelekezwa kwa Yesu, Yesu hakujielekezea Mwenyewe, ama Yeye hakujitambulisha Mwenyewe kwao. Kwa sababu, huwezi kumjua Yesu kwa njia hiyo. Yesu hajulikani kwa njia hiyo.

75 Lakini mara, tunaona hapa katika Maandiko, ya kwamba Wayunani hawa walipoleta, walipoletwa kwa Yesu, nao walikuwa Mbele Zake, inaonekana kana kwamba Yesu angalisema, "Vema, hili silo. . .Mimi—mimi ndimi Masihi wa jamii ya Kiyahudi, ambaye ametabiriwa na manabii, kwa uvuvio, kote katika karne nyingi. Nami huyu hapa sasa. Na mimi ndiye. . .nilizaliwa Nazareti. Mimi ni wa mama wa Kiyahudi. Baba Yangu ni Mungu. Nami nipo hapa sasa kujitambulisha Mwenyewe kwenu Wayunani." Sasa hiyo ingekuwa zaidi ni kama toleo lake la mwaka wa 1961.

76 Lakini, angalieni, mara walipoletwa Mbele Zake! Hilo ndilo jambo muhimu, wapeleke watu Mbele Zake. Na mara walipokuwa Mbele Zake, Yesu alisema, "Punje ya ngano isipoanguka ardhini ikafa, inakaa peke yake." Ni jambo lisilo la kawaida jinsi gani! Badala ya kukubali utambulisho wao, jambo alilofanya Yeye lilikuwa ni kuwaelekeza mahali wangaliweza

kumpata. “Punje ya ngano isipoanguka ardhini ikafa, inakaa peke yake.”

77 Yeye alifanya nini hapa? Aliwaelekeza kwenye ile Kweli kuu, jinsi ya kumwona Yeye. Wasingeweza kumwona Yeye katika njia ya Uzima wa Milele, akisimama tu pale jinsi alivyokuwa. Yeye alikuwa Mwanadamu.

78 Asubuhi chache zilizopita, niliona ono, yapata saa tatu ama nne asubuhi.

79 Nilikuwa nikimwomba Bwana, nikiuhisi wito sikuzote ukinisukuma kwa ajili ya nchi za kigeni mwaka huu, nianze mara moja, kote ulimwenguni. Ninataka kwenda Norway, pia nataka kwenda Ujerumani, Afrika, na mengi ya hayo mataifa, mwaka huu, Bwana akipenda. Wito tu moyoni mwangu, kwenda.

80 Nami nilikuwa nikimwomba Bwana, ndipo ono likaja machoni mwangu. Nami nilikuwa nimesimama wakati huo, nikatembea sakafuni na kuingia kwenye chu—chumba ambamo mlikuwamo na wanawake wawili, hasa. Mmoja alikuwa kwenye kaunta, na huyo mwingine alikuwa kwenye kaunta. Walikuwa wakiuza bidhaa mbalimbali. Vema, nikasimama kwa muda kidogo na kushangaa yote hayo yalihusu nini. Ndipo nikamwona mwanamume akiingia, naye akanunua kwa mwanamke kwenye kaunta *hii*, chupa ndogo ya manukato ya kumpelekea mwingine, mkewe, labda.

81 Ndipo nikaenda pale, na kusema, “Manukato hayo yanauzwaje? Ningetaka mengine kwa ajili ya mke wangu, bali ninataka ya lilaki. Napenda ya lilaki.”

82 Naye huyo mwanamume akasema, ama huyo mwanamke akasema, hasa, ninii . . . “Chupa hii ndogo ambayo mwanamume huyo alimnunulia mkewe, ni senti arobaini, bali sio lilaki. Chupa hii nyingine, ya lilaki, ni dola moja na senti tisini na nane.”

83 Nami nikasema, “Nitayachukua hayo.” Basi nikaenda kwenye pochi yangu, kutoa pesa. Nami nilifikiri nilimpa noti mbili za dola moja.

84 Huku akinirudishia, alisema, “Bwana, sizijui pesa hizi.” Ndipo akanirudishia. Nayo ilikuwa ni noti ya dola tano ya Canada.

85 Ndipo nikasema, “Kunradhi. Nilifikiri ilikuwa ni dola.” Nikasema basi, “Mimi ni . . . Mimi ni mmishenari. Nami, katika misheni zangu, ninapata fedha kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu. Na, katika hili, nimefanya kosa.”

86 Kwa hiyo, akanirudishia hiyo noti ya dola tano. Nami nikampa noti ya dola moja ya Kimarekani. Ndipo akanipa chenji, na akasema, “Ati mmishenari?”

Nami nikasema, “Naam, mama.”

87 Ndipo nilipokuwa nikizungumza, ama kumwangalia, alimwangalia huyo mwanamke mwingine, na kidogo akatikisa kichwa chake. Naye akasema, "Mpenzi, unaamini kwamba Ndugu Branham anasema kweli, kwamba sisi wanawake siku hizi itatubidi kuishi kama alivyotwambia, kuhusu kukata nywele zetu, na kuvaa mavazi yetu, na vitu kama hivyo?" Kasema, "Hivi hufikirii yeye amekosea katika hilo?"

88 Akasema, "Naam." Naye akasema, "Endelea, kipenzi. Wewe, Ruthu," ama chochote jina lake lilichokuwa; kasema, "unao uvuvio. Liseme."

89 Vema, upesi, nilijua nilikuwa katika ono, kwa hiyo nilijua ya kwamba hao walikuwa ni wanawake wawili, sikuzote. Mnaona? Hao ni, wote wawili, makanisa ya umoja na utatu. Hao hapo wamesimama pale.

90 Ndipo kasema, "Naam." Kasema, "Sidhani inatubidi. Kwa sababu, hatujawahi kuyaona macho Yake. Hatujawahi kuiona sura Yake. Tusingeweza kuijua sura Yake, kwa hiyo mbona tufanye hivyo?"

91 Nami nilikuwa na suti ya siku nyingi ya doria. Ndipo nikamwambia huyo mwanamke, nikasema, "Hebu kidogo, dada zangu. Mnaona, inawapasa tu kuishi kulingana na Biblia, haidhuru ilikuwa jinsi gani."

92 Akasema, "Lakini hatukuishi huko nyuma, wala hatujawahi kumwona Yeye."

Nikasema, "Mimi nimemwona." Kisha nikasema, "Jambo ni kwamba . . . "

93 Nikawazia, "Bwana, sasa, niko kati ya makanisa mawili, werevu. Sasa, huna budi kunipa hekima."

94 Ndipo basi nikajisikia nikiendelea kuzungumza. Ninataka mlichunguze. Sijawahi kuliwazia, maishani mwangu. Nikasema, "Mwanadamu siku hizi hana budi kuwa kama alivyokuwa wakati ule, kwa sababu yeye ni mwanadamu yule yule. Amefanyizwa kwa hisi tano. Na kama alisimama na kumwangalia Yeye, moja kwa moja usoni, bado ingembidi kuwa na hisi hiyo ya sita ya imani, apate kumwamini Yeye, haijalishi Yeye alionekana namna gani. Ingembidi kumwamini Yeye, kwa vyovyote vile."

95 Ndipo wakazificha nyuso zao kwa aibu, na kusema, "Kamwe hatukuliona, bwana, namna hiyo," wakaanza kuondoka. Ndipo nikageuka na nikaanza kwenda kwenye huduma za kimishenari, ambapo ninajua zilikuwa ni wi—wi—wito wa kurudi hudumani.

96 Sasa, mnaona, Yeye aliwaelekeza, hao hapo Mbele Zake, Kristo aliwaelekeza kwenye ile Kweli. Alisema jinsi ya kumwona Yeye, ilikuwa ni kuenda msalabani. Hapo ndipo ilipo, msalabani. "Punje ya ngano isipoanguka, inakaa peke yake." Basi kama Yeye hakufa, i—ingembidi kubaki peke yake, Mwenyewe, kama

hakufa. Lakini, Yeye, akiwa ni punje ya ngano iliyoanguka ardhini. "Halafu kama ikianguka ardhini," Yeye alisema, "itazaa mazao mengi, kama ikianguka ardhini ikafa." Kwanza, inabidi iwe ni punje iliyorutubishwa, la sivyo haitazaa chochote. Lakini haina budi kuwa na uhai ndani yake kabla haijaweza kuanguka ardhini. Naye alikuwa na Uzima wa Milele ndani Yake, kwa sababu Yeye alikuwa ni Imanueli. Naye ilimbidi kuutoa Uhai Wake Mwenyewe, apate kuleta Uzima tena.

97 Chukua, kama ngano. Unasema, "Punje moja ya ngano ingewezaje?" Hili hapa linalotukia. Punje moja inaanguka ndani, inazaa punje mia moja. Punje mia moja zinaanguka ndani, zinazaa punje elfu moja. Punje elfu moja zinaanguka ndani, zinazaa punje milioni moja. Punje milioni moja zinaanguka ndani, zinazaa be—behewa zima la shehena. Na kuendelea zaidi, na zaidi, na zaidi, mpaka inalisha ulimwengu mzima.

98 Hivyo ndivyo Yeye alivyomaanisha. "Kama nikiishi Maisha Yangu peke yangu, na nife hivi, niyaishi tu Maisha Yangu peke yangu, vema, basi, hakutakuwako na tunda baada Yangu. Bali nikianguka ardhini, chini ya mapenzi ya Mungu, basi nitaleta Kuzaliwa upya. Na katika Kuzaliwa upya huko, kutaleta kwingine pamoja na Kuzaliwa kupya, na kwingine pamoja na Kuzaliwa kupya, mpaka ulimwengu wote, utafanyiwa umishenari; Injili itahubiriwa." "Injili hii haina budi kuhubiriwa ulimwenguni kote, kwa ushahidi Kwangu. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

99 Kwa hiyo kama sisi wenyewe basi, katika huduma yetu, na katika mawazo yetu, na katika maisha yetu, kama tukikaa jinsi tulivyo, hatutafaa chochote. Inatupasa pia kufa madhabahuni, la sivyo tutaishi peke yetu; tutaishia dhehebu fulani ama kanuni fulani ya imani; tutaishia shirika fulani. Lakini tukifa kwa nafsi zetu, basi Roho Mtakatifu ataenezwa kila mahali, kwa midomo yetu. Hatuna budi kufa. Wengi sana, siku hizi, basi ni kama sasa. Ya kwamba iwapo. . .Hatuna budi kutambua kwamba inatupasa kufa, kusudi tupate kuzaa uhai mpya. Kwa hiyo Yeye alisema mengi sana katika hili, "Mkitaka kuniona Mimi, hamna budi kufa. Mfe kwa nafsi zenu, ndipo mtauzaa uhai mpya."

100 Sasa, tukitaka kumwona Yeye, kama kamwe ukitarajia kumwona Yeye, kamwe hutamwona kwa kujiunga na kanisa, kitabu fulani cha sheria unachokiweka, kanuni fulani za imani unazotumikia. Utamwona ukifa. Ukija Kalvari na usulubiwe kwa nafsi yako, basi utamwona Yesu. Tunataka kumwona Yeye.

101 Kwanza, kabla hajasema lolote, Yeye aliwaelekeza mahali pa kumpata. Kama vile Mataifa wote, ama watu wote, unampata Yesu msalabani, unaposulubishwa pamoja na Yeye.

102 Siku hizi, sisi hujaribu kumpata Yeye katika kila kitu. Tunajaribu kumpata katika jengo la kanisa. Tunajaribu

kumpata Yeye katika dhehebu. Tunajaribu kumpata Yeye katika kukariri kanuni fulani ya imani. Tunajaribu kumpata Yeye kwa kudumisha siku fulani, kwa kutii desturi fulani. Lakini hatuwezi kumpata, mpaka tutakapokuja Kalvari. Hapo tunasulubiwa, tunaanguka kwenye mavumbi ya ardhi, na kufa kwa nafsi zetu, kisha tunazaliwa mara ya pili. Ndipo tunampata Yesu.

103 Loo, wengi sana hujaribu, siku hizi, kujishikilia wenyewe na kushikilia wazo lako mwenyewe. "Nina njia *yangu* kwake. Ninaamini *hili*." Bali huwezi kumpata Kristo mpaka ufe kwa nafsi yako, na kumkubali Yeye, Neno, ndipo uupate Uzima. Hebu tuone.

104 Ni tofauti jinsi gani leo hii! Ni tofauti jinsi gani leo hii, leo hii, na makanisa, ama wanafunzi wa siku hizi! Wao wanafanya nini, ukiwaendea wanafunzi siku hizi?

105 Hao wanafunzi, kabla hawajafanya lolote, waliwapeleka hawa Wayunani moja kwa moja Mbele za Yesu. Na ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, itambidi Yeye kutenda vile vile leo hii kama ukiletwa Mbele Zake.

106 Wanafunzi siku hizi ni tofauti sana, siku hizi. Wanajaribu kukupeleka kwenye kitanda cha mtoto, ama hori, ama kwa Baba Krismasi, ama kwa kisungura kwa ajili ya Pasaka, ama kitu kingine, badala ya Kristo. Kamwe hawawaleti Mbele za Kristo. Krismasi siyo Kristo. La. Siku hizi, wanawaleta, mahali pengine, kwenye sanamu fulani, kanisa fulani, dhehebu fulani, sheria fulani za kimafundisho, bali kamwe hawakuleti Mbele za Kristo.

107 Mwanafunzi halisi wa kweli angekuleta moja kwa moja Mbele za Kristo. Na kutoka hapo, Kristo atakuonyesha yale yaliyokubidi kufanya.

108 Sasa, "Roho imetoka kwenye Krismasi," mtu fulani alisema leo hii. Niliwasikia kwenye redio, kasema mtu aliyekuwa akitoa hoja, mhudumu fulani, kuhusu, "Watu wengi sana siku hizi wakisema, 'Krismasi si *hiki*. Nasi hatupaswi kuwa na Baba Krismasi na kadhalika.'" Ndipo jamaa huyo akajaribu kuelezea hoja zake vizuri, kwamba, "Kama ulimwondoa Baba Krismasi kutoka Krismasi, uliiondoa roho yake." Uliondoa roho ya Baba Krismasi, hiyo ni kweli. Nayo roho ya Baba Krismasi siyo . . .

109 Baba, hadithi fulani ya kubuni ya Ujerumani, mapokeo ya Ukatoliki wa Kijerumani, sio roho ifanyayo Krismasi. Roho Kristo aliyoelekeza kwake ni Roho Mtakatifu, ambaye si sherehe, bali ni ibada ya Mungu aliye hai.

110 Bali yeye alisema, "Ukimtoa Baba Krismasi, hakuna tena roho katika Krismasi." Ungeweza kuwazia mhudumu akisema hivyo hewani? Lakini hivyo ndivyo alivyosema, kasema, "Mwondoshe Baba Krismasi, nawe hunayo tena roho ya Krismasi." Vema, huenda ikawa, ukitumia neno *misa ya Kristo*, huenda usiwe na mengi ya hayo.

111 Lakini wewe mwondoe Baba Krismasi kutoka maishani mwako, uufungue moyo wako na kumwacha Kristo aingie ndani, uyafie mambo haya ya ulimwengu, kusudi uwe na Krismasi iliyo halisi. Naam.

112 Ni tofauti kabisa, jinsi ilivyokuwa, bali imebadilika. Sio—sio, Kristo hajabadilika. Wanafunzi wa siku hizi ni tofauti sana na wanafunzi wa kale. Siku hizi, wanafunzi huwaleta wasemaji, ama watafutaji, hasa, badala ya . . . Wanafunzi wa kale walimleta mtafutaji Mbele za Mungu. Na siku hizi, wanafunzi wa siku hizi, huwaleta mbele ya shirika fulani la kanisa, shirikisho fulani, kanuni fulani ya imani, mafundisho fulani, badala ya kuwaleta Mbele za Kristo.

113 Tulichukue neno *Krismasi*. Ni kwa nadra sana unapata kusikia Jina la Kristo likitajwa. Hulisikii likitajwa. Taa na vivutio vyote viko kwenye Baba Krismasi, sio kwa Kristo, hata ni vigumu kwa watu kujua Krismasi kweli inahusu nini. Wameifanya tu ya kikafiri na kuifanya ya kikafiri sana, mpaka yote imekuwa ni upagani. Ni siku kuu mno ya biashara ya sherehe. Sasa, kama wanataka kufanya siku ya biashara kama vile siku ya mama, ama siku ya baba, ama siku ya mwana, ama siku ya binti, hiyo ni sawa. Lakini ondoeni hiyo biashara kutoka kwa Krismasi. Niliona ubao si muda mrefu uliopita, uliosema, "Mrudisheni Kristo kwenye Krismasi."

114 Sasa, wanakuleta kwenye kanisa fulani, unajifunza kanuni ya imani. Wanakuleta kwenye Krismasi, unafanya nini? Unamwona Baba Krismasi. Wanakuleta kanisani, unaona dhehebu.

115 Bali Kristo aliwaleta msalabani. Na unapompata mwanafunzi halisi atakayekuelekeza kwa Kristo, Kristo atakuleta msalabani, ambapo unasulubishwa pamoja na Yeye. Nao Uzima Wake wa Milele na uhai wako vinakutana pamoja, nao uhai wako unakufa, nawe unauchukua Uzima Wake wa Milele, ndipo wewe ni mwana wa Mungu. Amina.

116 Ni tofauti jinsi gani, kati ya mwanafunzi wa kale na mwanafunzi wa siku hizi!

117 Kama ukimgusia mwanafunzi, "Ningependa kumjua Bwana Yesu."

118 "Vema, sasa angalia, sisi ni wafuasi wa kanisa *fulani-fulani*, shuka ukaungane na hilo, uungane nasi." Mnaona? Ama, "Tulikuwa . . . Sisi ni wanachama wa shirika *fulani* hili, basi njoo ukajiunge na *hilo*." Na hayo ndiyo unayosikia.

119 Lakini Kristo Mwenyewe aliwaelekeza watu kwa mauti Yake, na akasema, "Punje ya ngano isipoanguka ardhini, inakaa peke yake."

120 Loo, jinsi ilivyo tofauti! Naam, bwana. Jinsi ilivyo tofauti! Bali maisha yako na Uzima Wake hupatana, sio kanisani, sio

katika jengo, sio katika kanuni ya imani, sio katika matendo mema, bali msalabani ambapo unasulubiwa pamoja na Yeye. Hapo ndipo unapompata Kristo. Humpati Yeye kwa kufanya vema zaidi, kufungua ukurasa mpya. Kuanza maisha mapya, humpati Kristo. Unampata Kristo katika mauti pekee; sio katika hori, sio katika kuungama. Kuamini katika kanuni fulani za imani na hekaya, humpati Kristo huko.

121 Mtumishi wa kweli hukupeleka Kwake, na Yeye ni Neno. Unasema, "Basi, Ndugu Branham, kama Kristo yuko duniani leo hii, mtumishi halisi angempeleka Kwake, Kristo." Vema, Kristo yupo hapa, katika umbo la Neno. Nalo Neno huleta Uzima, kwa sababu Yeye ni Neno. Kristo ni Neno. Naam, bwana. Yeye ni Neno, Mwenyewe. Mtumishi wa kweli sikuzote hukupeleka kwenye Neno.

122 Sasa, Yeye ni Neno. Yeye ni Biblia iliyofanywa hai. Basi unapokufa kwa nafsi yako, pamoja na Kristo, kama vile punje ya ngano, basi Neno linaishi ndani yako, linaleta matokeo yale yale kama liliyoleta kwenye Ile punje hai ya ngano iliyopaswa kuanguka ardhini. Amina. Ninyi ni washiriki wa kufufuka Kwake. Ninyi ni washiriki pamoja Naye, katika baraka Zake zote, katika madhihirisho Yake yote. Ninyi ni washiriki pamoja na Yeye, katika yote Yeye aliyofanya.

Sasa, Yeye ni Neno na fasiri Yake ya kweli.

123 Sasa mnasema, "Loo, tunaiamini Biblia, bwana. Tunaamini Biblia."

124 Lakini sasa, kama mnaamini Biblia, Yesu alisema hili katika Biblia, Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Hiyo ndiyo fasiri ya kweli ya Biblia, kwa kuwa Mungu Mwenyewe yuko ndani yako, akirejesha fasiri Yake mwenyewe. Utukufu! Hiyo ndiyo fasiri ya kweli, Mungu ndani yako, akiyafasiri Maneno Yake mwenyewe. Amina. Hivi Yesu hakusema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio"? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mungu ndani yako, akitoa fasiri Yake mwenyewe. Haikulazimu kumwangalia mtu mwingine. Useme, "Neno linasema *hivi*." Liamini, Nalo litajifasiri Lenyewe, kwa kuwa ni Mungu akikutumia wewe kulifasiri Neno Lake mwenyewe. Amina. Kristo ndiye fasiri iliyo hai ya Neno Lake mwenyewe.

125 Hebu tuangalie baadhi yake, jinsi Yeye anavyolifasiri Neno, sasa, kama Yeye anayo fasiri ya kweli.

126 Sasa tunashuka hapa kwa Wamethodisti, wao wanasema, "Tunayo fasiri ya kweli." Wabaptisti, wanasema, "Tunayo fasiri ya kweli." Presbiteri, "Tunayo fasiri ya kweli." Church of Christ, linavyojiita, "Tunayo fasiri ya kweli." Ati hayo yote yana "fasiri ya kweli"? Yote yanatofautiana, moja na lingine. Basi, kuna kasoro mahali fulani.

127 Sasa, jinsi pekee tunavyoweza kujua, ni kupata vile Yesu alivyowaambia wale Wayahudi jinsi ya kulifasiri Neno. Amina. Na kama Kristo alisema hivyo, hilo linalifanya kweli.

128 Wamethodisti wanasema, "Jinsi ndugu zetu wanavyolifasiri Hilo, lile baraza." Wabaptisti wanasema, "Jinsi tunavyolifasiri Hilo." Wapresbiteri wanasema, "Jinsi tunavyolifasiri Hilo."

129 Lakini ni vile Yesu alivyolifasiri Hilo, hiyo ni kweli. Hebu tuangalie jinsi Yeye anavyolifasiri Neno. Yeye alisema, "Nisipozitenda kazi za Neno la Baba Yangu, msiniamini." Hilo latosha. Hivyo ndivyo Yeye alivyolifasiri. Alisema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi ambazo nimefanya. Basi nisipozitenda kazi za Baba Yangu, msiamini, hata kidogo." Amina. Hilo latosha.

"Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya."

130 Sasa, hapana budi pawe na kitu fulani cha kweli na kitu fulani cha uongo. Ama, au, tunafanya nini? Tunachezea nini? Ni kwa nini, tunazunguka hapa, tukijifanya kuwa Wakristo, na kufanya *hiki, kile*, na *kinginecho*, na kujiunga na kanuni *hizi* za imani, na kupeana mkono pamoja na Pentekoste ya namna *hii*, ama *ile*, ama Methodisti, ama Presbiteri, ama Baptisti, ama Katoliki? Yote hayo yanahusu nini? Tunafanya nini, kucheza mchezo wa ficha kifutio, paka na panya? Kwani tuko wapi?

131 Basi kunayo njia moja tu, msingi mmoja pekee. Kunayo njia moja tu ya hakika, hiyo ni fasiri ambayo Yesu alilipa Neno. Haleluya! Hiyo ndiyo fasiri iliyo sahihi. Kasema, "Nisipozifanya kazi ambazo Mungu alisema ningezifanya, basi msiniamini Mimi." Amina. Hiyo ndiyo fasiri.

132 Fasiri siku hizi ni, Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi zile zile nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Nayo Maandiko pia yalisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Yesu alisema, "Hiyo ndiyo njia ya kujua kama nilitoka kwa Mungu ama la." Hiyo ndiyo njia ya kujua.

133 Wao walisema, "Sasa, ngoja kidogo. Tunaye Ibrahimu, baba yetu." Yeye akasema, "Baba zetu walikula mana nyikani."

Naye Yesu akasema, "Wote wamekufa."

"Tulikunywa maji kutoka kwenye mwamba uliopigwa."

"Nao wote wamekufa."

134 Kasema, "Lakini Mimi ndimi ule Mkate wa Uzima uliotoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni." "Wala si Mimi ninayenena, ni Baba Yangu anayeishi ndani Yangu. Yeye ndiye Mfasiri wa Neno hilo la Kiungu. Naye anathibitisha tena kwamba Yeye ni Mungu, kwa sababu Yeye anafanya moja kwa moja pamoja na Mimi yale Yeye aliyosema angefanya." Amina. Hayo ni Maandiko.

135 Huo ndio Ujumbe wa kuwapelekea watu; sio kitanda kidogo, sio hori. Krismasi haitajwi katika Kitabu chote cha Biblia. Hakuna wakati hata mmoja Yesu aliwahi kuwarejesha kwenye kuzaliwa Kwake, bali kwenye mauti Yake.

136 Hakuna hata wakati mmoja Yesu aliwahi kusema, "Jiunge na kanisa." Hakuna hata wakati mmoja Yeye aliwahi kusema, "Ikaririni kanuni ya imani."

137 Bali Yeye alisema, "Njoni Kwangu." Naye alisema, "Yeye ajaye, kazi nizifanyazo Mimi zitafuatana naye vile tu zinavyofanya Kwangu."

138 "Kwa kuwa nisipozifanya kazi za Baba, msiniamini. Maana, Neno lilisema, Masihi ajapo, mambo haya yangetukia. 'Atakuwa ni nabii.' Naam. 'Atakuwa ni nabii. Atakuwa mwonaji kama Musa.' 'Viwete watarukaruka kama ayala. Vipofu wataona. Viziwi watasikia. Nao bubu watazungumza. Ingeonyesha, ndani Yake, jinsi Yeye angefanya ishara za Masihi.' Sasa, kama ishara za Masihi haziithibitishi huduma Yangu," Yeye alisema, "basi msiniamini Mimi. Lakini, hivi ndivyo unavyolifasiri Neno." Akasema, "Kama sina ishara hizi, basi msiamini. Lakini kama nikizifanya hizi ishara, nanyi hamwezi kuniamini Mimi nikilifasiri Neno, ziaminini hizo ishara, kwa kuwa zinanena juu ya Neno." Hiyo ndiyo fasiri halisi ya Hilo. Hiyo ndiyo. Huo ndio Ujumbe.

139 Haikubidi kuchuka neno la mtu yeyote. Haikubidi kujiunga na kanisa lolote. Huwezi kujiuga na Kanisa. Unaweza kujiunga na haya madhehebu. Lakini Kanisa la Mungu, unazaliwa ndani Yake, kutoka Kalvari.

140 Sema, "Mungu asifiwe! Hata nami, pia, Ndugu Branham." Basi kazi alizofanya Yesu, utazifanya pia. Ndivyo Yesu alivyosema. Mnaona? "Kazi nizifanyazo . . . " Ati nini? Alisema, "Kazi nizifanyazo, zinanishuhudia Mimi." Haleluya! "Kazi nizifanyazo, zinatoa ushuhuda." Hivi hamwoni? Kwa maneno mengine, "Ishara za Masihi, hivi hamwezi kuona yale Masihi alikuwa afanye? Nanyi hamwamini ninayo fasiri ya kweli ya Neno, basi ni kwa nini Baba Yangu anaiunga mkono? Mnafikiri Mimi ni mgumu sana kwa madhehebu yenu," Yeye akasema, "endapo mnafikiri Mimi ni wa kimsingi kupita ki—kiasi. Nanyi mnasema mimi ni 'mwendawazimu,' mimi 'nina pepo,' nimerukwa na akili."

141 Walimwambia Yesu kwamba Yeye alikuwa ni mwendawazimu. *Mwendawazimu* linamaanisha "mwenye kichaa." "Wewe una kichaa. Wewe si wa makundi yetu. Nawe uko hapa nje kama mwendawazimu. Umerukwa na akili."

142 Ndipo Yesu angeweza kuwaambia, jambo hili, "Basi kama ninyi ni wa Mungu, ziko wapi ishara za Mungu? Kama mlimwamini Musa, ziko wapi ishara za Musa pamoja nanyi? Kama mliwaamini manabii, ziko wapi ishara za manabii pamoja

nanyi? Kwa hiyo kama hamwezi kuamini ya kwamba Mimi nina fasiri ya kweli, ziaminini zile ishara, kwa kuwa Hizo zinashuhudia kwamba niko sahihi." Haleluya! "Hizo ndizo zinazonishuhudia Mimi. Zinatoa ushuhuda kama niko sahihi au sivyo. Wote alionipa Baba wataifuata Hiyo na kuja Kwake. Wala hakuna mtu atakayeweza kuja asipoitwa na Baba." Kweli.

143 Hata hivyo, "Alikuwa amefanya kazi nyingi sana," Biblia ilisema, "hata hivyo wasingeweza kumwamini, kwa sababu Isaya alisema, 'Wanayo masikio wala hawawezi kusikia; macho wala hawawezi kuona.'" Wao ni vipofu kama popo. Hata hivyo, hawawezi kuliona, kwa sababu nabii alisema wasingeweza. Sasa, ni jambo lile lile leo kama ilivyokuwa wakati huo. Naam.

144 Kasema, "Kama hamwezi. . .Sizifanyi kazi. Si Mimi nizifanyaye, niyasemaye hayo Maneno. Si Mimi nizifanyaye hizo kazi, vinginevyo. Ni Baba Yangu. Na kama mnajua kile Mungu alichokuwa, Mungu alikuwa Muumba. Mungu Ndiye aliyekuwa juu ya Musa, naye Mungu ndani ya Musa akatabiri siku Zangu. Mungu alikuwa katika Agano la Kale," Yeye alisema. Ni kama kusema, "Yule aliyekuwa juu ya manabii, aliwaambia ya kwamba, 'Yule Nabii Mkuu atakuja siku moja, na Kwake watoto watakusanyika.' Kama hamwezi kuamini vile ninavyowafasiria Neno, basi iaminini ishara, kwa kuwa zinanena habari Zangu."

145 Loo, wasingeweza kuamini. Wao, wasingeweza kuliona Hilo. Yeye alikuwa Mungu katika mwili. Kwa sababu, Yeye alikuwa ni nini? Alikuwa ni Neno lililodhihirishwa. Alikuwa kile Mungu alikuwa ameahidi.

146 Sikilizeni, enyi Maskani ya Branham. Jiwekeni tayari kuingia kazini, kwenye usiku huu wa mkesha wa Krismasi. Mnaona?

147 Kama Yeye hakuwa, basi Mungu asingalimthibitisha. Bila shaka. Kwa maneno mengine, Yeye angeweza kusema, "Ni lipi kati ya makundi yenu (Mafarisayo, Masadukayo, ama chochote walicho), ni yupi wa watu wenu, ni kuhani mkuu wenu yupi, mwanachuoni wenu yupi, ambaye Mungu humtumia kunena Neno Lake kupitia kwake na kulidhihirisha, kusema Hilo ni kweli?"

148 Vema, wangesema, "Watu wetu wameelimika. Sisi ni werevu. Tunaijua Biblia hiyo kutoka kizazi kimoja hata kingine."

149 "Vema, basi, kwa nini Mungu halifanyi liishi tena katika watu hao, iwapo ni Neno la Mungu?"

150 Angalieni. "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja," sio watatu. "Sisi ni Mmoja." Mungu yuko ndani Yake. Mungu hunena kupitia Yeye. Yeye si mali Yake mwenyewe tena, bali Yeye ni Sauti ya Mungu kupitia kwa midomo ya binadamu. Haleluya!

151 Na kila mwaminio ndani Yake, usiku wa leo, vivyo hivyo amemilikiwa, amemilikiwa sana, amejitolea kabisa, mpaka maneno yake yanakuwa kama Maneno ya Kristo. Yeye hunena nalo hilo Neno linafanyika mwili. Ananena nalo hilo Neno linadhihirishwa. "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

152 Isaya alisema, katika mlango wa 42, ndio kwanza tusome, "Nuru kuu imekuja." Nuru! Loo, sitaki kuliondokea hili somo. Lakini Nuru kuu kuliko zote iliyowahi kuangaza iliangaza ndani ya maskini yule Mnazareti, mnyenyekevu: Mtu asiye na uzuri wowote hata tumtamani; Mtu asiye na elimu, tukinena kilimwengu; Mtu asiyejua taratibu za ibada za dini na mambo ya ulimwengu huu. Lakini angeweza kuwafunga pepo, kuwafufua wafu, nao pepo wakatetemeka.

153 Naye Mungu akamtambua kutoka Mbinguni, na akanena, "Huyu ni Mwana Wangu mpendwa." Sio mbele ya watawala matajiri, bali mbele ya kundi teule alilokuwa ameliita. Nuru kuu!

154 Mbona? Nuru kuu ilikuwa ikimulika kutoka kwenye Neno Lake. Neno lilikuwa ni nini? Kristo. Yeye alikuwa ni nini? Neno lililofanywa Hai. Nalo Neno lililofanywa Hai, lilitoa Nuru kuu zaidi kuliko Yeye alivyofanya hapo aliposema, "Na iwe nuru," katika Mwanzo 1. Hiyo ilikuwa ni nuru ya uumbaji, uumbaji upatikanao na mauti, ambao hauna budi kuanguka. Bali Neno Lake lilikuwa ni Uzima wa Milele na Nuru ya Milele. Basi wakati mtu alipoamini Hilo, yeye alikuwa na Nuru ya Milele.

155 "Nuru kwa wale waliokaa katika maeneo ya vivuli vya mauti," Mathayo 4. "Kuleta Nuru kwa Mataifa," ambao walimilikiwa na kuhukumiwa na Mungu, katika sanamu zao. Lakini Yeye akaja kama Nuru.

156 Alisema nini? "Neno Lako ni Taa ya njia yangu, Nuru ya kuimulikia njia ya miguu ya—yangu, kuniongoza."

157 Na leo hii, Nuru ya Mungu ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, Nuru iliyodhihirishwa. Nuru ni kazi za Mungu, zilizonenwa na Neno la Mungu, lililofanywa Hai, nayo ni Nuru kuu zaidi kuliko ilivyokuwa mwanzoni mwa uumbaji. Amina. Nuru kwa taa, kwa njia. Jamani! Ee Mungu! Nuru, lile Neno!

158 Katika giza kama tulivyo siku hizi, tumejawa na kanuni za imani na madhehebu, tumejawa na mihemko na ulokole, mioyo iliyofunguliwa kwa makaburi ya kila namna ya roho, ambayo hata ingelikana Neno hili kwamba ni la Kweli, na kusema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, manabii, na kadhalika. Walikufa, miaka mingi iliyopita."

159 Kisha kumwona Mungu, katikati ya giza, giza la kanuni ya imani, giza la madhehebu, akilichukua Neno Lake na kundi la

watu ambao wataliamini Hilo, na kuangaza Nuru Yake na Uzima Wake. Ni Nuru zaidi. Ni Nuru ya Milele, zaidi ya vile ilivyokuwa mwanzoni mwa uumbaji. "Iwe nuru; ikawa nuru." Bila shaka.

160 Sasa, Yesu kamwe hakusema, sasa, Yeye atawapeleka Bethlehemu. Yesu kamwe hakuwaambia hao Wayunani, walipomjia, "Sasa, hebu kidogo tu. Mkitaka kumwona Huyo, nitawarudisha Bethlehemu ambapo nilizaliwa. Nami nitawaambia jinsi ilivyotukia huko nyuma." Haikuwa hivyo.

161 Aliwaelekeza kwenye mahali pa siku za usoni, iwapo walitaka kumjua Yeye. "Mkitaka kunijua Mimi," kwa maneno mengine, "Sitawarejesha nyuma na kuwaambia wakati nilipozaliwa huko Bethlehemu, na yote kuhusu hayo. Nitawaelekeza mahali ambapo nitasulubiwa kwa ajili yenu. Na hapo ndani, kama mtasulubiwa pamoja na Mimi, na kuchukua msalaba wenu na kunifuata Mimi, mtajua Mimi ni Nani. La sivyo, kutoka hapo, hamtajua hilo kupitia kwa sanaa zenu za kale. Kamwe hamtajua."

162 "Vema," unasema, "Ndugu Branham, lakini tunajifunza Hilo kupitia kwa sanaa ya Biblia." La. Hatufanyi hivyo. Kama tukilijua kupitia kwa sanaa ya Biblia, basi kwa nini Mafarisayo hawakuwa Nalo? Halijulikani kupitia kwa sanaa ya Biblia, maana kunao wanasanaa wengi kupita kiasi wanaojaribu kulitia rangi. Lakini Biblia ni ya kweli, bali Mungu ndiye Mwanasanaa.

163 Kanuni za imani siku hizi zinasema, "Jiunge na *hili*. Kariri wimbo *huu* wa sifa. Rudia Kanuni ya Imani ya Mitume. Jiunge na kanisa letu. Peana mikono. Batizwa, jina la 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.'" Hizo ni kanuni za imani za kimadhehebu. Kweli. Mwanasanaa hakuitia picha hiyo rangi hivyo.

164 Mwanasanaa aliitia rangi, kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele. Kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hivyo ndivyo Mchoraji alivyolitia rangi. Kwa hiyo wakati Mungu anapoliakisi hilo, unajua umeipata picha iliyo sahihi. Nje ya hilo, una nakala bandia. Amina. Ichukue maskini nakala hiyo bandia, ya namna fulani ya kanuni ya imani, ukakitupe kitu hicho nje ya mlango, usiku wa leo. Kisha uchukue Nuru ya Injili ya Biblia, na uache Mchoraji amtie Kristo rangi ndani yako. Amina. Hiyo ndiyo njia. Ndivyo hivyo.

165 La, Yeye kamwe hakuwapeleka horini. Hakuwapeleka kwenye Krismasi.

166 Isaya alisema, "Ataitwa Jina Lake. . . " Katika mlango ule ule, yeye alisema, "Ataitwa Jina Lake. . . " La, mlango wa 55 wa Isaya. Alisema, "Ataitwa Jina Lake wa Ajabu, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele." Amina.

167 Laiti ningalikuwa na wakati. Ninapaswa kuwa nao. Ningetaka kuchukua somo juu ya kila moja ya hayo: "Mshauri,

Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, na wa Ajabu."

168 Hebu tuligusie tu wazo la wa Ajabu, kwa dakika moja, wa Ajabu. Loo, Isaya alisema Yeye alikuwa ni wa Ajabu. Hebu tuwazie baadhi ya mambo aliyosema, yaliyomfanya Yeye wa Ajabu. Ni kitu gani kilichomfanya Yeye wa Ajabu? Wakati aliposema jambo hili, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja," wa Ajabu.

169 Niambie ni Farisayo gani angaliweza kusema hilo. Niambie ni kuhani gani mkuu angaliweza kusema hilo, huku Mungu akimuunga mkono. Mnaona?

170 Kasema, "Nisipozifanya zile kazi sasa, msiamini lolote ninalosema. Bali nikilihubiri hili, basi inaonyesha ya kwamba Mungu alinituma kulifanya."

171 Kasema sasa, ndipo Yeye akasema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja." Sio, "Mimi na Baba Yangu ni watatu." Yesu alisema. Sasa, kanuni ya imani inasema, "Mimi na Baba Yangu ni watatu." Bali Biblia ilisema, naye Yesu akasema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja." Hiyo ni Ajabu. Mnaona jinsi Mungu, "alivyofanyika mwili"? Haleluya! Sio mtu wa pili, ama wa tatu, ama wa nne; bali Mungu Mwenyewe. Yesu alisema hivyo. Hebu bishana na Yeye, si na mimi. Ninasema tu yale Yeye aliyosema. "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Si Mimi ninayetenda hizi kazi. Ni Baba Yangu. Yeye anaishi ndani Yangu. Msiponiamini Mimi; aminini Neno, sababu Yeye ni Neno. Naye Neno akafanyika mwili, nami Ndimi. Hapo mwanzo alikuwako Neno."

172 Mwandishi yule yule wa Injili, Yohana, alisema, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu."

173 Hilo linamfanya Yeye na Mungu Mtu yuye yule; kama Mungu ni Neno, na Yeye ni Neno. "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja," basi. Loo, hilo ni Ajabu! Naam, bwana.

174 Mambo mengi sana tungeweza kusema juu ya hilo, Ajabu, mambo aliyosema Yeye!

175 Jambo lingine alilosema, "Mimi ndimi Nuru ya ulimwengu." Niambie kasisi angaliweza kusema hilo. Niambie dhehebu linaloweza kusema hivyo. Niambie kanuni ya imani inayoweza kusema hivyo. Hilo ni Ajabu.

176 "Mimi ndimi Kweli." Loo, jamani! Kanuni zetu za imani ziko maili milioni moja kutoka kwenye Kweli. Kanuni ya imani haiwezi kumfanya Mungu adhihirishwe. Kanuni ya imani haiwezi.

177 Ni kama tu vile Eliya alivyosema, juu ya Mlima Kameli, "Kama Mungu ni Mungu, hebu na ajibu." Kanuni ya imani haitafanya hivyo. La, bwana.

178 Bali Mungu atafanya hivyo. Mungu ni nani? Neno, Neno lililodhihirishwa. Atafanya hivyo.

179 "Mimi ndimi Nuru ya ulimwengu. Mimi ndimi Kweli iliyo katika ulimwengu. Mimi ndimi Njia." Hakuna njia nyingine ila Yeye. Hivyo tu. Usipitie kwenye kanuni ya imani. "Njoni Kwangu." Mnaona? "Mimi ndimi Njia, Nuru, Kweli." Yote hayo, Yeye alikuwa. Hayo ni maneno ya ajabu aliyoyasema. "Mimi ndimi Njia. Mimi ndimi Kweli. Mimi ndimi Nuru. Mimi ndimi—Mimi ndimi wa Kwanza; Mimi ndimi wa Mwisho. Mimi ndimi Mwanzo; Mimi ndimi Mwisho. Mimi ndimi Yule aliyekuwako, aliyeko, na atakayekuja. Mimi ni Shina na Uzao wa Daudi. Mimi ni Nyota ya Asubuhi. Mimi ni Alfa na Omega. Mimi ni Yote. Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Yeye anaishi ndani Yangu. Mimi ni Yeye. Yeye ni Mimi."

Wao walisema, "Wewe, ukiwa ni Mwanadamu, unajifanya mwenyewe Mungu?"

180 Loo, kama vile alivyowaambia Mafarisayo wakati mmoja, "Mnakosea, kwa kutolijua Neno la Mungu, wala nguvu za Mungu. Mnakosea, kwa kutolijua." Hakika. Maneno ya ajabu! Ajabu!

Hebu tuwazieni juu ya kazi za ajabu, wakati mmoja. Yeye alifanya nini?

181 Yeye alikuwa ni nini? Isaya alisema atakuwa ni wa Ajabu. Wakati alipoanza kumwita majina yote angaliweza, "Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele," yote haya, yeye alisema, "Yeye ni wa Ajabu." Maneno ya Ajabu!

182 Sasa tutazungumza juu ya kazi za ajabu, kwa dakika moja. Ni kazi gani alizofanya zilizokuwa ni za ajabu?

183 Siku moja kulikuwako na msafara wa mazishi ukitoka Naini—Naini. Mjane mmoja, akiwa na mwanawe wa pekee, amekufa, amelala kwenye kilili cha jeneza, amekauka, maiti, ametiwa dawa asioze, akishuka kaburini kuzikwa. Yeye alikuwa amesafiri kote kutoka Nazareti. Miguu yake, inauma, imejaa mavumbi, amechoka, amedhoofika. Akasikia kilio hicho. Akaangalia. Akishuka barabarani, akaja maskini mjane, anaomboleza. Mvulana wake, mwanawe wa pekee, amelala kwenye hiyo machela, amekufa.

184 Ikawa, pale, kwamba alipitia mahali Yesu alipokuwa. Mauti na Uzima hayawezi kukutana, mwajua; moja haina budi kuondoka. Akasema, "Simamisheni mbebaji." Akajongea pale na kumgusa huyo mvulana. Ndipo uhai ambao—ambao ulikuwa katika mvulana huyo, ambao ulikuwa umeondoka labda siku mbili, ukamrudia. Ninaweza tu kuona sanda ikianza kusogea, nawaona watu wakianza kutazama. Ndipo mtu aliyekuwa amekufa, akasimama kwa miguu yake, akaenda na kumkumbatia mama yake, labda. Hizo ni kazi za Mungu. Ajabu! Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika zilikuwa.

185 Ninaweza kumwona Yairo, maskini kasisi mmoja, alikuwa ni mtu mzuri. Yeye alimwamini Yesu, bali ilibidi atulie, kwa ajili ya wenziwe.

186 Waaminio wengi sana wa kisiri siku hizi kama huyo, wanahofia watafukuzwa kanisani mwao. Mnaona? Waoga, Mungu hawezi kuwatumia hao. Mungu anataka mtu ambaye anaweza kusimama pale. Hata ikimgharimu mauti, kulitia muhuri. "Msimwogope yeye ambaye huuangamiza mwili, bali Yeye auangamizaye mwili na kuipeleka nafsi kuzimuni."

187 Yairo. Ninamwona akienda nyumbani mwa huyu—huyu mhudumu. Akaenda ambapo mtoto mdogo, wa pekee, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, maskini msichana mdogo amelazwa mkavu, mfu, amelazwa kwenye machela. Mwili wake mdogo, usio na uhai ulilazwa pale. Maskini mikono yake, iliyokwajuka. Makucha yake yalikuwa yamekuwa meupe. Midomo yake ilikuwa imebonyea. Homa ilikuwa imemwua, ama kitu fulani. Macho yake madogo yamekakamaa na yamejifunga, na kitu fulani kilikuwa kimewekwa juu yao, labda. Maskini nywele zake zilikuwa zimechanuliwa. Kulikuwa na waridi na kadhalika yamewekwa karibu naye. Naye mama na baba, wakipiga mayowe. Majirani, wanapiga mayowe. Mtoto wake wa pekee alikuwa ameondoka.

188 Ninamwona akiingia kwenye chumba hicho. Amina. Akaangalia kote. Akawaona wote. Ndipo wakaanza kumcheka. Akawaondoa chumbani. Hilo ni Ajabu. Mnaona? Mtu mmoja anaweza kudhibiti umati wote. Kwa nini hawakusema kitu? Waliogopa kusema jambo.

189 Kwa nini hawalihukumu Neno siku hizi? Wanaogopa kusema hivyo. Hivyo tu.

190 Akaingia kwenye chumba hicho, akaushika maskini mkono huo baridi, akanena kwa lugha isiyojulikana, huko nje mahali fulani. Ndipo roho ya mtoto huyo ikamrudia, naye akaishi tena. Kazi za ajabu! Naam, zilikuwa hivyo. Zilikuwa ni kazi za ajabu, zilithibitisha kwamba Yeye alikuwa ni wa Ajabu.

191 Huenda pia nikasema juu ya Lazaro, walipokuwa tayari wameutia dawa mwili wake usioze, siku nne hapo kabla, wakaweka safu baada ya safu ya viungo juu yake, na kumzungushia kijana mwanamume huyu nguo tena na tena. Naye huyo hapo, amelala kaburini, na ameoza. Pua yake tayari ilikuwa imebonyea. Midomo yake ikabonyea usoni mwake. Mabuu ya ngozi yalikuwa yameanza kumla. Nayo nafsi yake ilikuwa imeenda safari ya siku nne, huko nje mahali fulani.

192 Ninamwona, maskini mabega Yake, yaliyoinama. Loo, jamani! Ulimwengu ungalisema, "Tazameni hicho. Mwangalieni Mtu huyo. Mwangalieni. Nanyi mlimwita Yeye, Mungu. Huyo hapo, akishuka kwenda kaburini, akilia machozi ya kibinadamu." Biblia ilisema ya kwamba Yeye alilia. Machozi

yakitiririka mashavuni Mwake, akivuta pumzi, akielekea kaburini. Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati huo.

Lakini ninamwona Yeye akisema, "Liondoeni jiwe." Amina. Amina.

193 Akabadilisha mandhari. Lazaro, aliyekuwa amekufa siku nne, akasimama kwa miguu yake akaishi tena. Ninaweza kuona kiungo kikianza kuipenya blanketi ambayo alikuwa amefunikwa. Kitu gani? Uhai ulikuwa umeingia tena. Harufu mbaya ilikuwa imetoweka. Mwili mpya ulikuwa umekuja. Roho, iliyokuwa mahali fulani siku nne, ikarudi mwilini mwake, naye mtu akasimama kwa miguu yake. Nena kuhusu kuwa wa Ajabu, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, huyo hapo. Hakika, alikuwa hivyo. Vema.

194 Tunamwona yule mwanamke kisimani, wakati Yeye aliposimama na kuzungumza naye dakika chache, na kumwambia ya kwamba alikuwa na waume watano wakati huo. Akasema, "Bwana, hapana shaka Wewe ni nabii. Tunajua, ajapo Masihi, hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake."

195 Akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye." Wa Ajabu! Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wa Ajabu!

196 Usiku mmoja bahari ilikuwa ikinguruma. Yeye alikuwa amelala, kutokana na uchovu, kama tu mwanadamu. Alikuwa amelala, kutokana na uchovu. Pepo walikuwa wameapa wangemzamisha usiku huo. Nao walidhani karibu tu walikuwa wamempata, wakati matanga yalikuwa yemeraruka, makasia yamevunjika, mtumbwi ulikuwa umejaa maji na kufurika. Wakarudi nyuma haraka, hao wanafunzi, wakasema, "Si kitu Kwako kwamba tunaangamia?"

197 Naye akasimama, akapangusa usingizi kutoka machoni Mwake. Kasema, "Loo, enyi wa imani haba, nitakuwa nanyi kwa muda gani?"

198 "Utafanya nini sasa? Utafanya nini huku nje kwenye bahari hii yenye dhoruba wakati hii, Galilaya kubwa, inazama moja kwa moja chini kwenye kila wimbi? Utafanya nini, wakati ibilisi ametandaa kwenye ule mlima huko ng'ambo, akiyanong'onezea hayo mawimbi namna hiyo, akitupa hayo?" Amechoka, mwajua. Mwajua, Yeye huko chini. "Inayarusha hayo maji juu, futi thelathini ama arobaini kwenda juu. Utafanya nini?"

199 Kasema, "Nitakuwa nanyi muda gani?" Akaweka mguu Wake juu ya demani ya mtumbwi na kusema, "Amani, tulia." Ndipo upepo ukanyamaza. Kwa maneno mengine, Yeye alisema, "Upepo, funga kinywa chako. Mawimbi, rudini chini mahali penu." Hapakuwapo hata na kiwimbi juu ya maji. Akasimama pale na kuangalia kote.

200 Akarudi nyuma, huku kundi la mitume walioshangaa sana limesimama pale. Akalala tena, akaendelea na usingizi Wake.

201 Wakasema, "Ni Mtu wa namna gani huyu?" Wa Ajabu! Amina. Wa Ajabu!

202 Hivi hamwamini Yeye alikuwa ni wa Ajabu? Hakika. Alikuwa ni wa Ajabu. Naam, bwana. Wakati, Mtu huyo Mwenyewe alitoka Mbinguni, huku mfumo wote wa jua ulikuwa ni taji Yake, kila bilioni moja ya nyota zilizoning'inia ardhini, kila nyota. Hayo mamilioni ya maili huko ng'ambo, wakati wanapoangalia kupitia darubini hiyo, huko ng'ambo kwenye Mlima Palomar, na wangeweza kuona maili mia moja ishirini ya uwazi wa nuru, na mabilioni hayo yote na matrilioni ya nyota yalikuwa kwenye taji Yake. Na Yeye akaziacha, apate kuchukua taji ya miiba. Ni nani angeweza kufanya hivyo? Ajabu! Loo, jamani!

203 Milele ilikuwa ndiyo joho Lake. Alikuwa amevikwa Uzima wa Milele. Kamwe hakuwa na mwanzo. Hakuanza Bethlehemu, mwajua, kama vile watu wanavyojaribu kuwazia alianzia. Hakuwa na mwanzo. Amina. Alivikwa Uzima wa Milele, kisha akausukuma kando, apate kuchukua joho chakavu na chafu la mauti, kwa ajili yako na yangu. Wa Ajabu! Uhu-huh.

204 Mbingu zilikuwa Ikulu Yake. Mbingu yote ilikuwa ni Yake. Hiyo ilikuwa Ikulu Yake. Hakuna kitu kingaliweza kamwe kunawiri pamoja na Yeye. Na Yeye akaja duniani. Na hata akasema, "Mbweha wana matundu, na ndege wana viota, bali mimi hata sina mahali pa kukilaza kichwa Changu." Hiyo ni ajabu. Sivyo?

205 Enyi marafiki, nina muktadha mwingi sana uliondikwa hapa. Lakini labda sina wakati wa kuupata. Nitaharakisha.

206 Huyo ndiye yule Yesu unayepaswa kumwona. Si Yesu wa kimadhehebu wanayenena habari zake; si Yesu wa kanuni za imani; si Yesu wa namna fulani ya hadithi ya kubuni ya Krismasi; si Yesu fulani wa kisungura fulani cha Pasaka; bali yule Yesu wa Kalvari, Yesu Yule aliyeweka kando kila kitu, Ambaye manabii walinena kumhusu.

207 Tungeweza kuendelea mbele hapa, "Baba wa Ajabu, wa Ajabu, Baba wa Ajabu, Mshauri wa Ajabu, Mfalme wa Amani wa Ajabu, Mungu wa Ajabu Mwenye nguvu." Tunazidi tu kwenda, kwenda, kwenda. Mnaona? Lakini kuweka kando, tunasema hivi, "Hatuna budi kuona, ikiwa wewe...Huyo ndiye Yesu ambaye hatuna budi kumwona, kupata Uzima Wake wa Milele."

208 Huwezi kuupata katika kanuni ya imani. Huwezi kuupata katika kujiunga na kanisa. Huwezi kuupata kwa namna fulani ya hekaya ulizohadithiwa, Baba Krismasi. Baba Krismasi hana Uzima wa Milele. La. Kanuni ya imani haina Uzima wa Milele.

209 Sio kulijua Neno Lake, hata kukupa; kulijua, Hilo halikupi Uzima wa Milele. "Kumjua Yeye," Biblia ilisema, "kumjua Yeye, ni Uzima wa Milele." Sio kulijua Neno Lake. Kumjua Yeye!

210 Wayunani walitaka kumwona. Walitaka kujua utu Wake. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu."

211 Sasa, huoni kwa macho yako. Unaona kwa moyo wako. Unaona? Unaangalia kwa macho yako. Unafahamu kwa moyo wako. *Kuona* ni "kuelewa." Unaangalia kitu fulani moja kwa moja, unasema, "Sikioni." Lakini, unakiangalia. Lakini, unamaanisha, "hukielewi" hicho.

212 Wayunani walitaka kumjua Yesu, Naye akawapa njia ya kumjua. Kumjua Yeye! Sio kuijua kanuni Yake ya imani, sio kulijua Neno Lake, sio kuijua miujiza Yake, bali kumjua Yeye! Na njia pekee unayopata hilo, ni msalabani, sio kwenye kitanda kidogo. La. Msalaba ndio ninaouona. Aliwaelekeza msalabani, sio kwenye. . .Sio kwenye kanuni fulani ya imani, ama—ama hori fulani, ama namna ya madhehebu, bali msalabani.

213 Na sasa ni vile vile siku hizi, mwanafunzi halisi, na kama ukiwahi kuja kwa Yesu. Yeye kamwe hatasema, "Yesu aliniambia kwenda kujiunga na kanisa *fulani-fulani*." Kamwe hakufanya hivyo. Asingelifanya leo hii. La.

214 Ukitaka kumwona Yeye, atakuelekeza msalabani. Nenda kule upate kufa, kisha utamjua Yeye, kama ukitaka kumjua.

215 Hata wakati mmoja Yeye hakumwelekeza mtu yeyote kwenye kanuni yoyote ya imani, dhehebu lolote, wala kwenye kuzaliwa Kwake, wala hata kwenye Krismasi. Hakuna hata wakati mmoja Yeye aliwahi kufanya hilo. Ningekaa kwenye hilo kitambo kidogo, lakini si—sitakaa. Hata hivyo, kama si muhimu, kama Yesu. . .Huwezi kulipata popote katika Biblia, ambapo aliwahi kumwelekeza mtu yeyote mahali pengine popote, kumjua Yeye, ila msalabani. Hiyo ni kweli. Na huko ni kujisulubisha mwenyewe. "Mtu asipozaliwa mara ya pili." Halafu, ikiwa lile hori, Baba Krismasi. . .

216 Yesu kamwe hakuandika kanuni ya imani. Hakuchagua dhehebu. Basi ni kwa nini tunalitilia uzito namna hii, na hata kuweka kila jukumu juu yake? Ninataka kuwaulizeni hilo; Krismasi, sasa. Ni kwa nini basi makanisa yetu yanaweka uzito sana kwake, kwamba, "Huna budi kuwa mfuasi wa kanisa *hili*. Huna budi kukariri kanuni *hii* ya imani. Huna budi kufanya *hivi, vile,* ama *vinginevyo*"? Ni kwa nini tunalitilia uzito hivi, kama si muhimu? Inaonyesha tuna wanafunzi wa aina nyingine tofauti na tuliokuwa nao. Wanataka kuwaleta kanisani mwao, kwenye dhehebu lao, ama kwenye kanuni yao ya imani, wala siyo kwa Kristo.

217 Watu siku hizi, kama wakiulizwa, "Wewe ni mwaminio?" Nimeuliza hili, mara nyingi. "Wewe ni mwaminio?"

218 Wanasema, "Loo, mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mmethodisti." Vema, hiyo inaonyesha wewe si mwaminio basi. Mnaona? Hiyo ni kweli. "Baptisti, Pres-. . ." Lakini unasema, "Mimi ni Mpentekoste." Hilo halina uhusiano wowote nalo. La, bwana.

Mwaminio ni kiumbe kipya. Lakini hapo ndipo wamelifikisha, siku hizi. Mnaona? Wanafanya hivyo kwa nini? Ni kitu gani kinachowafanya watu waseme hivyo?

219 Hivi majuzi usiku, nilikuwa hospitalini. Nilikuwa nikitaka kumwombea maskini mwanamke aliyekuwa mgonjwa. Akaponywa. Nami nikasema . . . Palikuwapo na mtu na mama yake wameketi pale. Nadhani alikuwa ni mama yake. Naye alionekana kama mama yake. Nami nilikuwa nikizungumza na mama huyo. Nikasema, "Tutaomba sasa."

Ndipo nikageuka, "Mnajali kama tukiomba?"

Akasema, "Vuta hilo pazia."

Nikasema, "Vema, niliuliza tu kama ungejali kama tukiomba."

Akasema, "Sisi ni Wamethodisti. Vuta hilo pazia."

220 Nikasema, "Basi hili lingekuogopesha hata kufa. Afadhali nilivute pazia basi, unaona." Nikasema, "Kama wewe ni Mmethodisti tu, basi wewe si Mkristo. Kwa hiyo nitaninii tu . . . " Naam.

221 Kwa nini wanasema hivyo? Mwanafunzi fulani wa uongo aliwapeleka tu umbali huo. Hayo ndiyo yote wajuayo, mwanafunzi fulani aliyefunzwa vibaya. Wanafunzi wa Yesu waliwapeleka kwa Yesu. Mwanafunzi wa Kimethodisti huwapeleka kwa Methodisti. Mbaptisti huwapeleka kwa Baptisti. Nao Wapentekoste huwapeleka kwa Wapentekoste. Bali mwanafunzi wa Kristo huwapeleka kwa Kristo, naye Kristo huwapeleka Kalvari. Hilo ndilo jambo halisi. Naam, bwana. Naam, bwana.

222 Huo ndio umbali walioletwa. Wameletwa tu umbali huo. Mnaona? Kama wa—wakisema, vema, "Mbaptisti, ama Mmethodisti, ama Mpresbiteri, ama *nini*," huo ndio umbali wote ambao wameletwa, "Katoliki," chochote kilicho. Huo ndio umbali wote walioletwa, kwa hiyo hayo tu ndiyo wanayojua.

223 Lakini, Mungu ashukuriwe, wanafunzi hawa walimjua Yesu. Kwa hiyo wakampeleka kwa . . . Wakawapeleka Wayunani hawa mahali walipojua ni pa Kweli. Basi mwanafunzi halisi wa Kristo, aliyewahi kumpata Kristo, humpeleka m—mtafutaji moja kwa moja kwa Yesu. Naye Yesu anawaelekeza Kalvari, ambako wanakufa pamoja na Yeye na wanazaliwa mara ya pili, upya. Loo, jamani! Huo ndio umbali waliomo.

224 Lakini, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Hilo lilikuwa ndilo swali. "Hatutaki kuona kanuni ya imani. Hatutaki kuwaona Wamethodisti. Hatutaki kuona Baptisti. Hatutaki kuona yeyote wa hawa. Tunataka kumwona Yesu." Lakini shida ni nini?

225 Sina budi kufunga tu, ndugu zangu. Sikilizeni kwa makini sasa, matamshi machache tu hapa kabla hatujafunga. Kitu gani?

Ninataka hili lieleweke kabisa sasa, nikiweza, kukishindilia kitu hicho kabisa.

226 Hao Wayunani walitaka kumwona Yesu. Yeye hakumpata katika Krismasi. Hakumpata katika shirika fulani. Hakumpata katika kanuni fulani ya imani. Kamwe hakuwaelekeza kwa vitu kama hivyo. Mmelipata hilo vizuri? Lakini Yeye aliwaelekeza msalabani, wapate kufa, wapate kufa. Mwanafunzi halisi husema, "Huna budi kufa." Ninajuaje wakati nimekufa? Wakati unapolitambua Neno hili lote kuwa ni Kweli, ndipo Neno linapoanza kuishi ndani yako.

227 "Vema," unasema, "lakini kanisa letu linafundisha..." Sijali kile kanisa lenu linafundisha. Ni yale Biblia isemayo. Unakoenda, kanisa hilo lingine hufundisha jambo tofauti. Lakini Biblia hii inafundisha jambo lile lile.

228 Naye Yesu alisema, "Wakati wowote unapolikubali Neno hili, Neno hili litadhihirishwa ndani yako. Litafanya jambo lile lile linalosema litafanya ndani yako."

"Loo," wao wanasema, "siku za miujiza zimepita."

229 Nayo Biblia ilisema, "Yesu, yeye yule jana, leo, na hata milele." Utalifanyaje hilo litimie wakati Yesu aliposema, "Yeye aniaminiye Mimi," mahali papote, wakati wowote?

230 Marko 16 ilisema, "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Kwa muda gani? "Kote ulimwenguni." Kamwe hata haijafika huko bado, "Kila kiumbe." "Aaminiye na kubatizwa ataokoka. Asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Haya basi. Neno litafanyika Nuru. Litajiangaza Lenyewe.

231 Si kama ukienda kwenye kitanda kidogo na kusema, "Mtoto mchanga alizaliwa hapa, miaka mingi iliyopita." Upuuzi. Kila namna ya kanuni za imani na hekaya zinasimuliwa juu yake. Tunajua Yesu alijua kitu hicho chote kitaangamia, kitavurugika kabisa.

Bali kuna Kitu kimoja kisichovurugika, hicho ni Roho Mtakatifu.

232 "Loo," mmoja wao anasema, "Yeye alizaliwa papa *hapa*. Tunalo kanisa lililojengwa juu yake." Mwingine alisema, "Yeye amezaliwa *hapa*."

233 Kama vile, mnajua ni misumari mingapi waliyo nayo, wanaweza kuthibitisha, misumari asili iliyokuwa msalabani? Kumi na tisa. Kila jamaa akishika msumari. "Huu, *sisi* tunao. Haleluya, *sisi* tunao."

Wana mifupa iliyokufa tu ya wengine. "*Sisi* tunayo. *Sisi* tunayo."

234 "*Hapa* ndipo mahali Yeye alipozaliwa." Huyo mwingine anasema, "*Hapa* ndipo mahali Yeye alipozaliwa." Huyu

anasema, "*Hapa* ndipo mahali Yeye alipozaliwa." Inaleta tofauti gani?

235 *Hapa* ndipo mahali Yeye alipozaliwa, moyoni. Naam. Nilipokufa, Yeye alizaliwa *hapa* ndani. Nilizaliwa mara ya pili, ndani Yake, upya. Jambo ndilo hilo.

"Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Vema.

236 Vema, kuna shida gani? Yeye amepotea tena. Watu wamempoteza. Hiyo ni kweli. Lakini amepotea tena, kwenye umati mkubwa, umati wa kanuni za imani. Mnakumbuka wakati mmoja Yeye alipotea, kwa wazazi Wake? Amepotea tena. Alipotea.

237 Shuka kwenye mitaa hii, kama vile imekuwa siku chache zilizopita, uangalie umati wazimu, ukisukumana na kupigana kumbo, na kunywa pombe, na kulaani, na kushutumu. "Liza njuga, liza njuga." Kristo amepotea. Yeye hajapotea. Watu wamempoteza.

238 Walimpata wapi? Mahali walipompotezea. Hapo ndipo tutakapompata.

239 Lakini Yeye amepotea, katika kanuni zao za imani na katika umati wao. Yeye amepotea. Kristo amepotea, kwenye umati wa kibiashara. Umati wa kibiashara unasema, "Hatuna budi kuisherehekea Krismasi."

240 Mama mmoja alisema hivi majuzi, akisimama pale, wakati mimi na mke wangu tulipokuwa tumesimama pale. Kasema, "Nilimnunulia baba kisaga cha wiski."

241 Huyo mwingine akasema, "Vema, nitanunua . . . Nitakuambia nitakachomnunulia baba. Nitamnunulia karata na vibao. Tutacheza poka ya kujiambua, unaona, kuisherehekea Krismasi."

242 Wengine wakasema, "Ndio kwanza nimnunulie mama yangu katoni ya sigara. Ulimnunulia nini wewe?" Hum! Hum!

243 Ee Mungu! Yeye amepotea. Walimpoteza, katika Krismasi. Walimpoteza, katika Pasaka. Kisungura, ama kofia mpya; sio ufufuo, sio kuzaliwa kwa Kristo.

244 Walimpoteza, katika kanuni zao za imani, walipowafanya miungu watatu kutoka Kwake, wakamkata vipandevipande na kufanya sanamu, badala ya kujua kwamba Yeye ni nani. "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja." Mlimpoteza.

245 Yeye amepotea, katika umati wao wa kidini. Umati wa kidini ulimpotezaje? Amepotea, kwa kanisa Lake, katika Laodikia. Kanisa la mwisho, wakati wa kanisa, ilisema Yeye alikuwa nje ya kanisa, "akibisha," akijaribu kuingia ndani. Tamasha la kusikitisha sana katika Biblia nzima, ni hali ya kanisa katika siku za mwisho kabla Yeye hajaja. Hakuna wakati mwingine wa kanisa uliopata kumtupa Yeye nje. Hawakujua tofauti yoyote.

Sasa wakati kweli wanapojua nguvu halisi za Roho Mtakatifu, walimtupa nje ya mahali hapo, yuko nje, akibisha mlango. “Tazama, nasimama mlangoni nabisha.” Hakika.

Walimpoteza, katika umati wao wa kibiashara.

246 Walimpoteza, katika umati wao wa kidini. Hiyo ni kweli. Walifanya kanuni za imani kutoka kwake. Walifanya madhehebu kutoka kwake. Wakampoteza. Walichukua—walichukua desturi badala ya Biblia. Walichukua lundo la mawazo ya wanadamu badala ya yale Mungu aliyosema. Wakasema, “Weka jina lako kwenye kitabu. Peana mikono. Hivyo tu ndivyo mnavyopaswa kufanya. Kubatizwa, ‘Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.’” Kitu hicho chote ni cha uongo. Hiyo ni kweli.

247 Hapo ndipo umati wa kanisa ulipompotezea, walipompoteza. Kwa nini? Si katika majengo yao ya kanisa, sio katika kile-mnachokiita, ku—kundi lao la watu. Bali walimpoteza walipoliacha Neno. “Kama hiyo. . .Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo. Mtapewa. Mtatendewa, mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu,” maana ni Mungu, aliyefanyika mwili tena. Unaona? “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo. Mtatendewa.” Jambo ndilo hilo.

248 Lakini, siku hizi, hawakai. Wao ni, leo hii, Mmethodisti, kesho Mbaptisti, siku inayofuata Mpresbiteri, hawajafika popote bado.

249 “Neno Langu likikaa ndani yenu! Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.” Haleluya!

250 Ndugu Neville, hiyo ni kweli kabisa. [Ndugu Neville anasema, “Loo, utukufu! Ninajua hilo.”—Mh.]

Neno lililofanyika mwilini mwako, likinena kupitia wewe.

251 Wapentekoste walimpoteza. Loo, naam. Walikuwa na Yeye, miaka michache iliyopita, bali wakampoteza. Walifanyaje hilo? Kwa kuona ni nani angeweza kujenga jengo lililo kubwa kuliko yote, um-hu, ambaye angekuwa na kanisa lililo kubwa kuliko yote, kwaya iliyofunzwa vizuri kuliko yote.

252 Kama kuna kitu chochote ambacho sikipendi, ni sauti iliyofunzwa kupita kiasi, ambayo itasimama na kuimba kana kwamba wana ugonjwa wa utumbo mpana, hiyo “hwiii,” kushikilia pumzi yao mpaka wanakuwa weusi usoni. Hawaimbi. Wanapiga tu kelele.

253 Lakini kile ninachopenda ni mtu mzuri, aliyezaliwa mara ya pili, wa kipentekoste wa mtindo wa kale, aliyeguswa moyoni, wakiimba kutoka moyoni mwao. Kama hawawezi kubeba tuni kwenye ndoo, wangali wana Roho mle. Unaweza kumhisi Huyo akipenya mwilini mwako. Haleluya! Ninapenda hilo. Ninapenda hayo matokeo yake, Roho Mtakatifu akiubariki, mwajua. Naupenda huo. Huo ni halisi tu, kwangu mimi. Naam.

254 Ila walimpoteza. Kwaya zilizofunzwa vizuri na wahubiri waliofunzwa vizuri. Naam. Loo, jamani! Kila namna ya nywele zilizowekwa mawimbi, mwajua, na kuinamisha vichwa vyao *hivi*, wapate kupigwa picha. Na, loo, naam, wamefunzwa vizuri. Hakika wamefunzwa. Hao wamefunzwa vizuri.

255 Shule kubwa za Jumapili, hakika, kila kanisa likijaribu kulishinda hilo lingine, katika shule ya Jumapili. Nayo shule ya Jumapili hata haijanenwa habari zake, katika Biblia. Hilo ni fundisho la sharti la Methodisti. Kwanza iliitwa "shule ya matambara." Kila mtu sasa huenda kwenye shule ya Jumapili, ambao hawawezi kulingojea kanisa, kwa sababu walichukua kitu fulani mbali na kile Mungu alichosema. Kweli.

256 Kumbukeni, kamwe sikusema nilihubiri chochote chini ya uvuvio, maishani mwangu, kilichonibidi kughairi, kama nilivyofanya madhabahu, hivi majuzi, na kadhalika, mwajua, *Uzao wa Nyoka,* ama lolote la hayo. Hebu mtu fulani aje ayararue kwa Neno la Mungu. La.

257 Hapo ndipo walipompoteza; shule kubwa ya Jumapili, ama hema iliyo kubwa kuliko yote lililopo, watu waliovalia nadhifu kuliko wote mjini. Hiyo ni Pentekoste. "Mbona, sisi ni wafuasi wa kanisa la kwanza. Kundi lililo bora kuliko yote mjini huenda huko." Mashemasi, waliooa mara tatu ama nne, shemasi kwenye halmashauri, labda mchungaji, pia. Kila namna ya upuuzi makanisani siku hizi. Mnaona? Walifanyia wapi? Walimpoteza Yesu.

258 "Vema, mwajua, dhehebu letu ndilo kubwa kuliko yote katika Pentekoste. Wanaume wetu ndio wanaume waliofunzwa vizuri kuliko wote waliomo mle." Huenda wakawa yote hayo. Sikanushi hayo. Hayo yanaenda kwenye vyama na huduma za kithiolojia.

259 Bali ninataka kumjua mtu ambaye anamjua Yesu, amemwona Yeye na amezaliwa mara ya pili, nalo Neno linajiakisi Lenyewe katika neno lake. Unaweza kuona Hilo si lake. Naye amejitolea kikamilifu kabisa mpaka Kristo ananena kupitia yeye. Haya basi. Hiyo ni kweli. Nazo ishara na maajabu zinalifuata Neno hilo, kwa sababu Hilo ni Neno la Mungu.

260 Lakini kama Neno la Mungu likisema jambo fulani, nalo kundi *hili* liseme, "Loo, la. La, la. Dhehebu letu litatufukuza kama tukiamini Hilo." Basi amekwisha, papo hapo. Amejikatilia mbali, papo hapo. Hivyo tu. Unaweza ukachochea kitu fulani kimitambo. Unaweza kubuni namna fulani ya udanganyifu wa kimzaha, uwazie *hili, lile*, ama *linginelo*, lakini kile kitu halisi, cha kweli, hakipo hapo. Naam, bwana. Loo, hakika.

261 Makanisa, makanisa yanambadilisha Kristo kwa ulimwengu na kanuni za imani. Kanisa liko kwenye mpango wa ubadilishanaji. Loo, hakika wao wanataka ku—kubadilishana. Naam, bwana. Wataenda nao watabadilishana. Wanataka—

wanataka mpango wa ubadilishanaji. Wanataka kuyabadilisha yale Mungu asemayo, kwa yale dhehebu lisemayo. Wanataka kubadilisha yale Mungu asemayo, kwa "umfuate mchungaji." Wanataka kubadilisha yale Mungu asemayo, kwa "lifuate dhehebu." Wanabadilishana.

262 Mnajua nini? Watu wananunua. Loo, kuna biashara kubwa inayoendelea sasa. Ni Krismasi nyingine, ya bandia tu, ya kujibunia.

263 Laiti tungalikuwa na muda zaidi kidogo tu, nitarejea kwenye somo hili tena siku moja. Ninaruka mengi kupita kiasi hapa, ambayo Roho Mtakatifu alinipa muda mfupi uliopita. Mnaona?

264 Wakati kanisa linabadilishana, kanisa linatafuta, watu wanatafuta, wanaojiita kanisa. Naam, bwana. Wanabadilishana. Hakika wanatafuta na kubadilishana. Wanatafuta nini? Kanisa lililo kubwa kuliko yote, umati uliovalia nadhifu kuliko wote, dhehebu lililo kubwa kuliko yote. Nao hao watu. . . nitasema jambo fulani. Watu wanajaribu kutafuta, hata Wapentekoste, wanawake Wapentekoste wanajaribu kutafuta mahali ambapo watawakubalia kupita wakiwa na mambo zaidi ya ulimwengu: kaptura, nywele zilizokatwa, rangi. Wanafanya ununuzi.

265 "Mungu abarikiwe, mimi ni Mpentekoste. Haleluya! Mimi ni mfuasi wa *hili*. Na, loo, mchungaji wetu haamini. . . "

266 Mnaona, unayatafuta yale yatakayowaruhusu kuishi kichafu zaidi, (Mungu aturehemu), yale yatakayowaruhusu kuishi wachafu zaidi na kufanana zaidi na ulimwengu, wawezavyo. Wanatafuta kutoka mahali hadi pengine, wakimkataa Kristo. Hilo linaweza kusaga kama kila kitu. Limekusudiwa kufanya hivyo. Watu wanatafutatafuta. Wanafanya ununuzi wa Krismasi ambako wanaweza kupata bei nzuri. Watafuta mapatano ya bei!

267 "Vema, mimi ni Mpentekoste, pia. Vema, hatuna Upuuzi huo wa kale wa mawazo finyu." Lakini Biblia inasema hivyo.

Kama yeye ni mwanafunzi wa kweli wa Kristo, atakuongoza hadi msalabani.

268 "Loo, Ndugu Branham, nilitoka nikaenda na kuzungumza kwa lugha." Hilo halimaanishi chochote. Nyumbu alifanya hivyo, siku moja. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. . .

269 Simaanishi kufanyia mzaha Neno takatifu la Mungu. Ninaamini katika kunena kwa lugha.

270 Lakini ibilisi hunena kwa lugha. Watu wanaweza kunena kwa lugha na kuishi maisha ya namna yoyote. Bali, ninamaanisha, i—ibilisi ana na—nakala ya kila kitu Mungu alicho nacho.

271 Naye anaweza kuiga kila kitu ila Kuzaliwa halisi kwa Kristo, wala hawezi kufanya hivyo. Maana, huna budi kufa, kwanza, kisha Neno linakufufua. Unajuaje wakati ukiwa hai? Wakati Neno hilo, kila Neno Lake, limefanyika mwili ndani yako.

Kila kitu Biblia inachosema, unasema kitu hicho hicho, nacho kinatimia vile vile hasa Yeye alivyokisema. Hapo ni wakati ikiwa, naam, wakati wewe, wakati roho yako inapokubaliana na Yeye. Yeye ni Neno. Wakati roho yako inapokubaliana na yale Yeye aliyosema, naye Roho anajidhihirisha Mwenyewe kupitia kwa Neno Lake, basi wewe unaishi. Unaona? Umemaliza kutafutatafuta, basi, na kubadilishana, na hayo mengine yote. Yote yamekwisha. Naam.

272 Watu wanatafutatafuta, wapate mahali wanapoweza kuishi kilimwengu zaidi, Wapentekoste na wote. Msije, ninyi Wapentekoste, mkawadhihaki hao Wabaptisti na Wapresbiteri. Nyungu haiwezi kuiita birika chafu. La, bwana. La, hasha. Zote ni vile vile. Kwa hiyo wanatafutatafuta, wapate mahali wanapoweza kwenda kanisani na kujiunga na dhehebu, wapate kuwa maarufu, kuwaziwa vizuri mjini, meya wa mji huenda kwenye hilo kanisa. Ambapo, angeweza kwenda kanisani, azaliwe mara ya pili. Sasa, ninasema tu, wako mbioni, kanisa lililo kubwa kuliko yote mjini.

273 Ninawajua watu leo hii ambao ni wafuasi wa dhehebu dogo hapa juu barabarani, kanisa dogo, bali lilikuwa ni dogo sana. Kwa hiyo wakasema, "Kusudi watoto we—wetu waweze, nasi tunaweza, kuwaziwa vizuri zaidi kidogo," wakachukua barua yao kutoka kanisa moja wakashuka wakaingia lingine, dhehebu kubwa zaidi. Na mbali na hilo, hili lingine lilikuwa na sinema kwenye orofa ya chini, nao wangecheza karata na kila kitu namna hiyo, mwajua, na kucheza michezo hii, na kadhalika namna hiyo. Kwa hiyo wakawapeleka watoto wao huko chini. Walikuwa wameleta meza ya biliadi huko chini, mnaona, wapate kucheza biliadi, na kujiburudisha na mambo kama hayo. Kisha wawe na darasa la dakika kumi la shule ya Jumapili, na mapumziko ya kunywa kahawa, na mapumziko kusudi mchungaji aweze kuvuta sigara, kwenda nje. Loo, naam. Hiyo ni kweli. Nisingelisema hilo isipokuwa ninajua kile ninachozungumzia. Hiyo ni kweli. Loo, hakika. Mnaona?

274 Wanatafutatafuta. Kama wanaweza kuendelea na kuishi namna ya maisha wanayotaka kuishi, wafanye lolote watakalo, na bado waahidiwe Uzima wa Milele baada ya hapa, wanatafuta hilo.

275 Ninawaambia, iwapo mnataka kutafutatafuta, njoni pale Kalvari. Hilo latosha. Uifie nafsi yako chafu, dhambi zako, kisha uzaliwe mara ya pili, upya.

276 "Basi kama unapenda ulimwengu, au mambo ya ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Hiyo ni kweli.

Unasema, "Siamini katika utakatifu." Si ajabu, huwezi.

277 Lakini Biblia ilisema, “Pasipo huo, hakuna mtu atakayemwona Mungu.” Mungu ni mtakatifu. Kama Mungu anaishi ndani yako, wewe ni mtakatifu, pia.

278 Halafu uniambie unaweza kutoka kwenda kwenye karamu hizi, na kunywa kileo? Wapentekoste wengi hufanya hivyo, wanatoka wanaenda kwenye karamu hizi, na kuwapeleka hao wanawake huko nje na kuishi kwenye sehemu hizi, na kushuka na kujivua nguo, pamoja na mavazi ya kuogelea, na kwenda kuogelea mbele ya wanaume, wakati waume zenu, na ndugu, na dada, na kadhalika. Nao Wapentekoste wakitoka na mavazi ya kuogelea, na kujiita mwenyewe mshirika wa Bibi-arusi? Bibi-arusi wa Kristo hafanyi mambo hayo.

279 Loo, yeye anatafutatafuta, hakika, akitafuta njia rahisi, kisha aahidiwe Uzima wa Milele baada ya hapa.

280 Huna Huo, isipokuwa unaishi ndani yako, Neno la Mungu likiwa ni shahidi aliye hai kwamba Yeye yu hai, nawe ni hai ndani Yake. Loo, jamani! “Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu.” Loo! Sio kanuni hizi za imani, sio mambo haya ambayo watu wanajibunia. “Sisi tunataka kumwona Yesu.”

281 Lakini Yeye amepotea, kwao. Um-hu! Kwa nini? Hebu kidogo. Kwa nini? Kwa nini amepotea, kwao? Kwa nini Yeye amepotea, kwa Pentekoste? Kwa nini amepotea, kwa Mmethodisti na Mbaptisti? Kwa nini Yeye amepotea, kwa hayo madhehebu? Kwa sababu hawatachuka punje yao ya ngano na kuiangushia pale Kalvari, na kufa kwa kanuni yao ya imani, na kuzaliwa kwa Neno.

282 Kisha tunaoshwa kwa maji ya Neno, amina, tukawa viumbe vipya katika Kristo Yesu. Nazo ishara ambazo Kristo alisema zilimfuata Yeye, zitawafuata. Kila mwanamke atakuja mahali pake. Kila mwanamume atakuja mahali pake. Roho wa Mungu atakuja mahali Pake, nalo Kanisa la Mungu aliye hai halitakuwa na waa lolote. Hakika. Amina. Naam, bwana. Hivyo ndivyo inavyofanyika.

283 Hakuna mauti kwa punje yao ya ngano. Hawataliangusha dhehebu lao. Hawataliacha life. Laiti dhehebu la Kibaptisti lingaliangusha hiyo punje ya ngano ya Kibaptisti ardhini na kuiacha ife; laiti Methodisti ingeangusha punje yake ya ngano, laiti Assemblies of God, na Pentekoste Jina la Yesu, na Umoja, na Utatu, na yote mbalimbali, church of God, na hayo mengine yote, yangeiangusha punje hiyo ya ngano katika Neno; na kuiacha ife kwa mawazo yao wenyewe, na kuliacha Neno hili lidumu na kupata Uzima. Ndipo wangesema, “Msiponiamini mimi, aminini kazi nizifanyazo, kwa kuwa ndizo zinazonishuhudia mimi.”

284 Kazi hizo ni zipi? Yesu alisema, “Kazi hizi, kazi ambazo—ambazo Mungu alinipa kufanya. Na,” kasema, “kama Baba alivyonituma Mimi, nami nawatuma.” Kazi zenyewe ambazo Mungu alizifanya zilikuwa ndani Yake, zikamfanya Yeye na

Baba Mmoja. Nazo kazi zile zile ambazo Yesu alifanya, na Roho Mtakatifu wa Yesu ndani yako, atakufanya ufanye kazi zizo hizo. "Kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Hakika.

285 Wasingeiacha punje. . .Walifanya nini? Ni wafuasi waliokufa tu, waliokufa katika dhambi na makosa, waliokufa katika elimu, waliokufa katika mambo ya ulimwengu. Yana thamani kwao. Hiyo ndiyo sababu hawajazaliwa mara ya pili. Hiyo ndiyo sababu ishara haziwezi kufuata. Kwa sababu gani? Ni wafuasi waliokufa pekee. Hawana budi kuwa, mhudumu hana budi kuwa na Ph.D, na L. maradufu D., kabla hajaweza kuwa mchungaji wa baadhi ya makanisa. Na labda hajui herufi za kwanza za alfabeti, ABC, "daima mwamini Kristo." [Kiingereza: Always Believe Christ—Mf.] Kama alimwamini Kristo. . . [Ndugu Branham anaashiria—Mh.]

286 Jamaa fulani alinifuatilia, hivi majuzi, na kusema, "Kwa nini usiachane na hao watu, sikuzote unawakemea kuhusu jinsi wanavyovalia, mambo wanayofanya? Vema, kama wewe ni nabii. . . " Wao walisema, "Watu wanafikiri wewe ni nabii."

287 Nikasema, "Ninajua wamesema hivyo. Mimi siye. Lakini," nikasema, "wa—wa—walisema hivyo."

288 Kasema, "Vema, kama wanaamini kwamba wewe ndiye, basi kwa nini usiwafundishe jinsi ya kuona maono na kutembea mbele za Mungu?"

289 Nikasema, "Kama hawajui ABC, nitawafundishaje aljebra? Kama hawaijui shule ya chekechea, hawajui jinsi ya kujiadibisha, hawajui jinsi ya kuonekana na kutenda, na kuvaa nguo, na kuwa nadhifu, utawafundishaje mambo ya kinabii?"

290 Yesu alisema, "Kama hamyaamini mambo ya huku, mambo ya duniani, mtaaminije, kama nikiwaambia Mambo ya mbinguni?" Mambo ambayo mnaweza kufanya wenyewe, kuacha kufanya mambo haya. Hata hamwezi kufanya hayo, mtayapataje mambo ya kiroho, enyi watu? Hiyo si ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam, bwana.

Wamekufa tu, kwa elimu yao. Wanao umati wenye elimu.

291 Sasa nitafunga kwa kusema hili, maneno haya machache tu. Ujumbe wangu wa Krismasi, ni, hebu niwaelekeze usiku wa leo kwenye msalaba. Amina. Nanyi, enyi punje ya ngano, angukeni ndani ya Kristo kule mpate kufa. Humo mtapata Uzima Wake katika Neno Lake, akiwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Acha huo uwe ndio Ujumbe wangu wa Krismasi kwenu. Siwaelekezi horini, kwenye kitanda kidogo, kwenye kanisa, kwenye dhehebu. Lakini, "mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu," ndipo nitawaelekeza Kwake. Yeye anawaelekeza kwenye mauti Yake, kuzikwa na kufufuka. Nanyi muache punje yenu ya ngano ianguke mle ndani, na mliache Neno Lake liwe halisi ndani yenu, nanyi mtaona ya kwamba Yeye ni yule yule jana,

leo, na hata milele. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Na tuombe.

292 Baba wa Mbinguni, ingawa saa zinapita mbio, na Roho Mtakatifu anatenda kazi miongoni mwa watu, na kesho inapaswa kuwa ni ibada ya siku ambayo Wewe ulimtuma Mwana Wako wa pekee ulimwenguni. Nami nimejaribu, usiku wa leo, kutowaelekeza watu horini ambako Yeye alizaliwa, kwa kuwa Yeye alikuwa tu ni Mtoto mchanga wakati huo. Lakini ninajaribu kuwaelekeza kwenye kusudi ambalo Yeye alizaliwa, ili aweze kuwa Mwokozi wao, apate kuwa Mungu wao, Mfalme wa—wa—wa—wao, Yote kwa Yote kwao. Wapate kumjua Yeye Yule ajazaye nafasi yote, wapate kumjua Yeye; sio Yule aliyeanzia Bethlehemu, bali Yeye asiyekuwa na mwanzo, Yeye aliye Mungu wa Milele, ambaye angeweza kusimama duniani na kusema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja."

293 Ninajaribu kutenda kama mwa—mwanafunzi, vizuri nijuavyo mimi. Wakati watu walio na mioyo yenye njaa walipowaendea wale wanafunzi waliokuwa wa kweli, Filipo na Andrea, wao waliwapeleka Mbele za Bwana Yesu, na Yeye akawaelekeza kwenye mauti yaliyokuwa yanakuja, kusudi wapate kumjua Yeye na waweze kumwona.

294 Basi usiku wa leo, Baba, vivyo hivyo, ninawaelekeza Kalvari ambako Mwana wa Mungu, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, akauchukua mfano wa mwanadamu na akafanya maskani, akabadilisha umbo Lake, akatoka kuwa. . .Mungu wa Milele katika Utukufu wakati wa Milele alipofanyika mwanadamu na kupiga hema Lake miongoni mwetu na kufanyika mmoja wetu apate kuwa Mkombozi wa Jamii, kuturejesha kwenye ku—kumbukumbu la Mungu mwenye nguvu aliyetuumba.

295 Hapo Yeye akafa, pale Kalvari, na hapo hatuna budi kufa pamoja na Yeye. Kama Yeye alivyokufa, Mwana wa Mungu; kusudi tuweze kuwa wana wa Mungu, hatuna budi kufa pia, na kuacha punje yetu ya ngano ianguke ardhini pamoja na Yeye, maisha yetu yafe na kufichwa ndani Yake. Loo, kisha tufufuliwe katika kufufuka Kwake, kuendeleza kazi Yake, kumwacha Mungu Wake yeye yule, aliyekuwa ndani Yake, alete dhihirisho la Neno la Kanisa katika siku hizi za mwisho, kama Yeye alivyoahidi.

296 Mungu, tuna furaha sana kuona ya kwamba Yeye alithibitisha kila sehemu yake, kuonyesha ya kwamba Yeye ni Mungu. Yeye hulitimiza Neno Lake. Ile Nguzo kuu ya Moto ingali miongoni mwetu. Ishara kuu na maajabu ambayo Yeye aliahidi, zingali zinatendeka.

297 Ee Mungu, tuna furaha sana ya kwamba, usiku wa leo, ya kwamba kusudi lililomleta Yeye duniani, ya kwamba sisi

tunayo haki ya kuimiliki Roho Yake ndani ya maisha yetu. Hilo linatupatia Uzima wa Milele, Neno Lake lililofanyika mwili katika utu wetu wenyewe.

298 Na tujisalimishe wenyewe, usiku wa leo, Bwana, kujisalimisha kabisa, kwa kila kitu cha ulimwengu huu, tupate kufa kwa mambo ya ulimwengu; na kufufuka tena katika Maisha mapya ndani ya Kristo, tupate kupiga hatua katika mwaka huu ujao, kama huu mwaka ukiendelea hata mwisho, ama hata ukifika hapa. Bwana Yesu, tupate kuwa vyombo vipya vya Mungu, vilivyowekwa wakfu, vilivyooshwa kwa maji ya Neno, kupitia kwa Damu, na kutengwa kwa ajili ya utumishi wa Kristo! Tujalie, Bwana. Tunajikabidhi wenyewe Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Karibu na Wewe, karibu na Wewe,
Karibu na Wewe, karibu na Wewe;
Kote katika safari ya maisha ya msafiri,
Mwokozi, jalia nitembee pamoja na Wewe.

Hebu tuinue mikono yetu na mioyo yetu, tunapouimba.

Karibu na Wewe, karibu na Wewe,
Karibu na Wewe, karibu na Wewe;
Kote katika safari ya maisha ya msafiri,
Mwokozi, jalia nitembee pamoja na Wewe.

299 Na tuviinamishe vichwa vyetu na mioyo yetu, na kuuimba kwa utulivu; bali Kwake sasa, kana kwamba unamwangalia Yeye moja kwa moja.

Karibu na Wewe, karibu na Wewe,
Karibu na Wewe, karibu na Wewe;
Kote katika safari ya maisha ya msafiri,
Mwokozi, jalia nitembee pamoja na Wewe.

300 Ikiwa huo ndio ushuhuda wako, sasa inua mkono wako. Useme, "Karibu na Wewe! Kweli, Bwana, sio kanisa. Wewe! Sio kanuni ya imani, bali Wewe. Sio hori wala kitanda kidogo. Wewe! Ee Mungu, jalia Neno Lako liwe ndani yangu, nipate kuwa karibu na Wewe."

Kote katika safari ya maisha ya msafiri,
Mwokozi, jalia nitembee pamoja na Wewe.

301 Sasa wakati tukiimba tena, ushike, mkono wa mtu fulani, useme, "Nitakuombea, ewe Mkristo." Unaposhika mkono wao, hiyo ni kusema, "Nitakuombea, ewe Mkristo. Wewe niombee."

Karibu na Wewe, karibu na Wewe,
Karibu na Wewe, karibu na Wewe;
Kote katika safari ya maisha ya msafiri,
Mwokozi, jalia nitembee pamoja na Wewe.

Sasa wakati vichwa vyenu vimeinamishwa.

Katika hori zamani za kale, ninajua ni kweli kabisa,
Mtoto Mchanga alizaliwa awaokoe watu na dhambi zao.
Yohana alimwona ufukoni, Mwana-kondoo wa milele,
Loo, Kristo, Aliyesulubiwa wa Kalvari.

Karibu na Wewe, karibu na Wewe;
Kote katika safari ya maisha ya msafiri,
Mwokozi, jalia nitembee pamoja na Wewe.

302 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye si ni wa ajabu? ["Amina."]

Viwete walifanywa kutembea, bubu walifanywa kuzungumza,
Nguvu hizo zilinenwa kwa upendo baharini;
Vipofu walifanywa kuona, ninajua ingewezekana tu kuwa ni
Rehema za Mtu yule wa Galilaya.

Sasa, karibu na Wewe, karibu na Wewe;
Kote katika safari ya maisha ya msafiri,
Mwokozi, jalia nitembee pamoja na Wewe.

303 Hiyo ndiyo shauku yako usiku wa leo? Sema "Amina," kama ndiyo. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, ni ajabu jinsi gani!

Kote katika safari ya maisha ya msaf-. . .Sisi ni wasafiri.
Mwokozi, jalia nitembee pamoja na Wewe.

304 Mungu awabariki. Sio hasa "Krismasi Njema," bali baraka za Mungu za Krismasi ziwe juu yenu. Hebu Kristo wa Kalvari akufiche ndani Yake Mwenyewe, akufunike, akufunike sana na kukuvisha vazi la Neno Lake, mpaka Neno Lake litakapofanyika mwili ndani yako, ndilo ombi langu. Mungu awabariki. Mchungaji sasa, Ndugu Neville.

61-1224 Mabwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org